# HALI, HADHI NA MAJUKUMU YA SHENG MJINI NAKURU

**NA**

**FLORENCE WAIRIMU NJOROGE**

**Kazi hii imetayarishwa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili**

**(M.A) Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**Idara ya Kiswahili,**

**Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**2014**

# UNGAMO

Hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo chochote kile.

Florence W. Njoroge　　　　　　　　　　Tarehe

Tasnifu hii imetolewa na kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Dkt. Ayub Mukhwana　　　　　　　　　　Tarehe

Dkt. Jefwa Mweri　　　　　　　　　　Tarehe

## KUTABARUKU

Kwa babangu mzazi Lucas Njoroge na mamangu Margaret Wambui. Malezi yenu, upendo wenu, maombi na nidhamu mliyodhamini imekuwa dira yangu muda huu wote.

Wanangu wapendwa Naimalyne na Elvis.

Mpendwa wangu Duncan Ndungo.

Mapenzi yenu kwangu, maombi na uvumilivu zimenipa nguvu kuendelea na kazi hii.

## SHUKRANI

Ukamilifu wa kazi hii haungewezekana pasipo na mchango wa watu mbalimbali. Kwanza kabisa nampa mkono wa tahania Mwenyezi Mungu kwa kuniongoza kupitia roho wake na kuifanya ndoto hii kutimilika.

Shukrani zangu zingine ziiendee jamii yangu. Sijui niseme nini kwa wazazi wangu babangu mpendwa Lucas Njoroge na Mamangu Margaret Wambui ambao wamechangia kazi hii kwa maombi na kuilipa karo. Mwenyezi Mungu awabariki.

Shukrani zingine zimwendee mume wangu Duncan Ndungo na wanangu Naimalyne na Elvis kwa kuwa wavumilivu na kwa kutokuwa na wao wakati wanaponihitaji.

Siwezi wasahau dada zangu Fura, Shiro, Mendi, Wambui, Nyambura na Mukami kwa maombi yao. Mungu awabariki.

Dkt. Mukhwana na Dkt. Mweri wamekuwa wasimamizi wa kupigiwa mfano, ushauri wao umefanikisha utafiti huu. Mwenyezi Mungu awe nanyi siku zote za maisha yenu kwani mmekuwa manahodha wema.

Shukrani kwa wahadhiri wangu Prof. Habwe, Prof. Mwenda Mbatia, Dkt. Iribe, Dkt. Swale, Dkt. Mbuthia, Dkt. Jefwa, Dkt. Zaja na BW. Mungania mmekuwa viongozi wema Mungu awabariki. Mwisho nawashukuru wote waliohusika kwa hali yoyote ile, mlikuwa msaada kwangu wakati wote huo. Ijapokuwa sikuwataja kwa majina, nasema asante na Mungu awabariki.

## IKISIRI

Sheng imekuwa moja wapo wa lugha vipindi ambayo inatumika sana kwenye miji mingi nchini Kenya ukiwemo mji wa Nakuru. Matumizi ya lugha hii nyumbani, mitaani na hata shuleni umepelea lugha hii kukua na hata kuongeza misamiati na kuongezeka kwa watumiaji wa lugha hii. Utafiti huu ulilenga kutambulisha hali, hadhi na majukumu ya Sheng mjini Nakuru huku tukilinganisha Sheng na lugha nyingine zinazotumika mjini humo. Sababu ya kuteua mada hii ni kuona kuwa vijana wengi mijini wanatumia Sheng kama kitambulisho chao kilugha na haijatambulika kisheria. Malengo ya kazi hii nikutafiti kama Sheng ina majukumu maalum mjini Nakuru, kama hadhi ya lugha hii ni ya chini na kama kuna tofauti zilizoko katika matumizi ya Sheng kimaeneo. Ukusanyaji wa data kwa ajili ya utafiti huu ulifanywa kwa njia ya hojaji ambayo iliyafumbata maswala ambayo kwa kawaida hupelekea mtuamiaji wa lugha kuonekana kana kwamba ni mtu aliye na uelewa wa lugha tofauti mbali na kuonyesha hadhi zipewazo lugha mjini Nakuru. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia nadharia ya lugha na utambulisho wa jamii ya Gumperz na Cook (1982), nadharia chanzo cha ujifunzaji wa lugha ya pili ya Stephen Krashen (1989) na nadharia ya jumuishi na utambulisho ya Gile (1979). Uchanganuzi kutokana na nadharia hizi umeonyesha kuwa kila lugha huhusishwa na kikundi fulani cha wahusika na lugha hii huwa kama kitambulisho cha jamii husika. Kila lugha hupewa majukumu na hadhi kulingana na watumizi wake ni kina nani. Mbinu za ujifunzaji lugha pia huchangia katika kuipa lugha fulani majukumu na hadhi ya lugha husika. Sheng ni lugha ambayo ni kitambulisho cha vijana wa mijini nchini Kenya ukiwemo mji wa Nakuru.

# YALIYOMO


UNGAMO ... i
SHUKRANI ... iii
IKISIRI ... iv
YALIYOMO…....v
ISTILAHI MUHIMU…....vii
SURA YA KWANZA ...1
1.0 Utangulizi ...1
1.1. Usuli wa mada ...1
1.2. Tatizo la utafiti...4
1.3 Malengo ya utafiti...5
1.4 Nadharia tete...5
1.5 Umuhimu wa utafiti ...5
1.6 Upeo na mikakati ya utafiti ...6
1.7 Msingi wa nadharia...7
1.7.1 Nadharia ya lugha na utambulisho wa jamii...7
1.7.2. Nadharia ya chanzo cha ujifunzaji wa lugha ya pili ...10
1.7.3Nadharia ya jumuishi ya utambulisho ...14
1.8. Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti...15
1.9. Mbinu za utafiti...21
1.10. Uteuzi wa watafitiwa...21
1.11. Ukusanyaji wa data ...22
1.12. Vifaa vya ukusanyaji wa data...22
1.13. Uchunganuzi wa data ...22
SURA YA PILI ...23
LUGHA ZINAZOTUMIWA MJINI NAKURU ...23
2.0 Utangulizi ...23
2.1 Lugha ya Kiingereza ...23
2.2 Lugha ya Kiswahili...26
2.3. Lugha za Kienyeji...28
2.4 Lugha Vipindi Sheng na Engsh...29
2.5. Hitimisho ...32
SURA YA TATU ...33

HALI, HADHI NA MAJUKUMU YA SHENG MJINI NAKURU ....33
3.0 Utangulizi ....33
3.1. Hali na hadhi ya Sheng ....33
3.1.1 Sheng kama lugha vipindi. ....35
3.1.2. Hali na Hadhi ya Sheng Mjini Nakuru ....39
3.2. Majukumu na matumizi ya “Sheng” mjini Nakuru ....43
3.3 Majukumu ya Sheng ....48
3.3.1Sheng kamaKitambulisho cha Vijana ....48
3.3.2 Utambulisho ....48
3.4. Hitimisho. ....52
SURA YA NNE ....53
TOFAUTI YA MATUMIZI YA SHENG MJINI NAKURU ....53
4.0 Utangulizi ....53
4.1 Tofauti ya Matumizi ya Sheng Kijinsia. ....54
4.1.1 Matumizi ya Sheng kwa Jinsia ya Kike ....54
4.1.2 Matumizi ya Sheng kwa Jinsia ya Kiume ....55
4.2. Tofauti ya Sheng Kimaeneo Mjini Nakuru ....56
4.3.Mwelekeo wa wanafunzi kuhusiana na Sheng ....58
4.3.1. Mwelekeo wa Sheng kimajukumu ....58
SURA YA TANO ....64
HITIMISHO ....64
5.1 Utangulizi ....64
5.2 Muktasari wa matokeo ....64
5.3Pendekezo zaidi ....66
MAREJELEO……64
KIAMBATISHO A: HOJAJI ....71

**Istilahi muhimu katika kazi hii.**

| | | |
|---|---|---|
| Argoti | - | Slang |
| Daiglosia | - | Diglossia |
| Hadhi | - | Status |
| Isimijamii | - | Socialinguistics |
| Jumuia lugha | - | Language community |
| Kirioli | - | Creole. |
| Kitambulisho | - | Identity |
| Kukopa na kutohoa | - | Borrowing and Adaptation |
| Lingua Franka | - | Lingua Franca |
| Lugha | - | Language |
| Lugha kuu | - | High Language |
| Lugha msingi | - | Basic Language |
| Lugha rasmi | - | Official Language |
| Lugha vipindi | - | Slang. |
| Lugha ya kimataifa | - | International Language |
| Lugha ya taifa | - | National Language |
| Msimbo | - | Code. |
| Nadharia | - | Theory |
| Pijini | - | Pidgin. |
| Sera | - | Policy |
| TY | - | Tafsiri Yangu |

| | | |
|---|---|---|
| Ubadilishaji msimbo | - | Code switching. |
| Umenke | - | Gender |
| Umilisi | - | Competence |
| Umojalugha | - | Monolingualism. |
| Upangaji lugha | - | Language Planning |
| Upataji | - | Acquisition |
| Uwililugha | - | Bilingualism. |
| Wingilugha | - | Multilingualism. |

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

### 1.1. Usuli wa mada

Lugha ndio msingi wa mawasiliano katika jamii yoyote ile, kwa kuwa kila jamii huhusishwa na lugha fulani na kila lugha huhusishwa na jamii fulani. Hata hivyo, katika jamii iliyo na wingilugha; kila lugha huwa na hadhi yake kutegemea majukumu yaliyotengewa lugha hiyo. Msukumo ambao umenipelekea kuitafiti hali, hadhi na majukumu ya Sheng mjini Nakuru na ambayo ni lugha vipindi ni matumizi ya Sheng kama kitambulisho lugha kinachotumika sana miongoni mwa vijana kwenye miji mingi chini Kenya, Nakuru ukiwa mmoja wapo. Kitambulisho lugha hiki kinaendelea kukua na hata kuongeza misamiati kote nchini Kenya.

Sheng ni mfumo wa kiisimu ambao umekuwa tekelezi kwa wanaisimu pamoja na walimu wa Kiswahili katika shule za msingi na shule za upili. Mazrui (1995) anasema kwamba Sheng ni msimbo wa vijana ulioanza miongoni mwa vijana wanaotoka katika jamii zenye mapato duni kiuchumi wanaoishi kwenye mitaa ya mabanda mashariki mwa jiji la Nairobi. Maoni kama haya yamewahi kutolewa na Osinde (1986), Abdulaziz na Osinde (1997). Nadharia tete hii inaendelea kusema kwamba vijana wanaoishi na kulala katika nyumba yenye chumba kimoja cha kulala walibuni msamiati wa siri ili wazazi wao ambao pia walilala katika chumba hicho hicho wasielewe mazungumzo yao.

Kembo-sure (1992), pia anashikilia maoni yayo hayo na kusema kuwa sheng ni msimbo wa vijana wa rika moja. Wakati Abdulaziz na Osinde wanaposema kwamba Sheng

ilianza katika miaka ya sabini, kwa upande mwingine Mazrui na Mpande (1990) na Mazrui (1995) huku akimnukuu Michael Ngugi Karanja katika miaka 50 katika jela anasema kwamba huenda Sheng ilianza katika miaka ya thelathini na kwamba lugha hii ilianza miongoni mwa wezi wa mifuko kama msimbo wao wa siri.

Spyropoulos (1987:13), naye kwa upande wake anasema kwamba Sheng ilianza katika miaka ya hamsini na kushikilia kasi katika miaka ya sabini. Kinachomfanya Spyropoulos kusema hivyo ni kuwa maandishi mengi katika makala na majarida na katika magazeti kuhusu Sheng yalianza kuonekana katika miaka ya sabini. Hata hivyo haimaanishi kwamba huo ndio ulikuwa mwanzo wa lugha hii.

Kutoelewana huku kuhusu asili na chimbuko la Sheng kunamfanya Ngesa (2002) kudai kuwa hakuna asilia moja ya Sheng. Ifahamike pia kwamba madai mengineyo yapo. Hata hivyo, japo hakuna mwafaka kuhusu asili na chimbuko la Sheng, mambo yafuatayo yanaweza kudondolewa:

i. Sheng ni aina ya lugha na lugha hii inatumiwa na jamii fulani kuwasiliana baina yao.
ii. Wataalamu wengi kama vile Iribemwangi na Mukhwana (2011), Mazrui (1995), wanahusisha Sheng na vijana.
iii. Asili ya Sheng inahusishwa na watu wenye mapato duni katika jamii na wanaishi katika mitaa inayoakisi hali hiyo.
iv. Lugha hii pia inahusishwa na uhuni na wezi wa mifuko hasa katika miaka ya kuzuka kwake.

v. Sheng ilianza jijini Nairobi na kisha kuenea katika maeneo mengine ya Kenya na Afrika Mashariki kwa jumla.

Kwa sababu utafiti huu haulengi kushughulikia asili na chimbuko la Sheng, madhumuni hapa ni kuarifu kuhusu maswala hayo. Imekuwa vizuri kuonyesha ufahamu wetu wa mijadala tawala inayoendelea kuhusu lugha hii ambayo inazidi kuwa maarufu sana miongoni mwa vijana na kuenea kwa kasi mno.

Fromkin N.K (2003:487) anasema kuwa duniani kote na katika historia, watu wamebuni lugha ya siri na wametokea kuitumia lugha hii aidha kama kitambulisho mahsusi cha kikundi fulani ama kama njia ya kuwafanya wengine wasipate kuelewa kile kinachosemwa. Hapo awali lugha vipindi zilitumiwa haswa mingoni mwa vijana ili kukidhi mahitaji yao haswa ya kisiri. Lugha vipindi za Kenya ni lugha ambazo zinatumika hata kwenye vyombo vya habari kama redioni. K.m. kuna *Ghetto redio* ambayo hutumia Sheng kama lugha kuu kimawasiliano. Pia vipindi vimebuniwa vinavyotumia lugha ya Sheng k.m. kipindi cha *Bebabeba (NTV)* ambamo muhusika '*Tasha'* hupenda kutumia Sheng. Pia *Teke teke ndani ya churchil raw* ambamo muhusika *Ambuside* hutumia Sheng. Hivyo basi Sheng inajiendeleza kihadhi na hata kimajukumu kwa sababu lugha ambazo zilitumika hapo awali katika vyombo vya habari ni lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha asili za kiafrika.

## 1.2. Tatizo la utafiti

Katika maongezi ya kawaida lugha ambazo hutumika sana mjini Nakuru ni Kiingereza, Kiswahili na lugha asilia za kiafrika. Lakini miongoni mwa vijana lugha vipindi Sheng ni lugha ambayo wanaitumia katika mawasiliano yao ya kawaida, na pia katika kueleza mambo yao ya kisiri haswa wakati hawataki watu wengine waelewe wanachokizungumzia.

Imedhihirika katika sehemu ya usuli kuwa mijadala kuhusu Sheng imeegemea zaidi masuala ya asili na chimbuko la Sheng. Wengi wa wataalamu wameshughulikia sehemu ya isimujamii kuhusiana na Sheng hata hivyo kuna baadhi ya wale ambao wamejikita katika isimu pekee wakizungumzia muundo wa Sheng lakini kwa kijumla; miongoni mwao ni kama vile: Bosire (2008, 2009), Echessa (1990), Waithira (2002), Ogechi (2005). Ikiwa Sheng inatambulika kama lugha inayokua, inayoongeza misamiati yake kila uchao na kuenea kwa kasi katika miji nchini Kenya, kwa nini nafasi ya Sheng, hadhi na majukumu yake yasibainishwe kama ya lugha? Sheng ni muhimu kwa vijana mijini haswa mjini Nakuru kwa sababu wanaitumia kama kitambulisho lugha chao na pia wanajieleza na kuwasiliana kwayo bila woga na kujisikia kama sehemu muhimu ya jamii wakati wanaitumia na wenzao.

Utafiti wetu utaongozwa na maswali yafuatayo:-

1. Je, Sheng ina majukumu yepi katika mji wa Nakuru?
2. Hadhi ya Sheng ni ipi katika matumizi yake Nakuru na katika jamii nzima?
3. Kuna tofauti katika matumizi ya Sheng kimatumizi au kimaeneo mjini Nakuru?

### 1.3. Malengo ya utafiti

Utafiti wetu utaongozwa na malengo yafuatayo;

1. Kutambua majukumu ya Sheng mjini Nakuru.
2. Kuchanganua hali na hadhi ya Sheng katika mji wa Nakuru.
3. Kuchanganua kama kuna tofauti za matumizi ya Sheng kati ya wasemaji wa mji wa Nakuru.

### 1.4. Nadharia tete

1. Sheng haina majukumu maalum mjini Nakuru.
2. Sheng si ya hadhi ya chini mjini Nakuru.
3. Matumizi ya Sheng hutofautiana kimakazi na kimaeneo mjini Nakuru.

### 1.5. Umuhimu wa utafiti

Sheng ni moja wapo ya lugha vipindi ambayo inatumika sana mjini Nakuru. Vijana kati ya umri wa miaka 14 na 30 wanaitumia sana. Vijana hawa ndio viongozi wa kesho mjini Nakuru na nchini Kenya kwa ujumla.

Sheng haijatambulika kama kitambulisho lugha muhimu miongoni mwa vijana na kwa hali hii, swali linalotujia ni;

Ni kwa nini?

Kuzuka kwa lugha vipindi kama vile Sheng katika miji mingi nchini Kenya kumepelekea lugha hizi kupewa hadhi na majukumu hasa miongoni mwa vijana. Kwa mfano ni lugha ambayo wanaitumia katika maongezi yao ya kawaida, pia vijana hutumia Sheng kueleza

mambo yao ya kisiri haswa wakati hawataki watu wengine waelewe wanachokizungumzia.

Lugha hufumbata maswala yote ya jamii, hivyo basi ni kupitia matumizi ya lugha ambapo tunajifunza tamaduni za jamii zetu. Ni kupitia lugha ambapo imani na mawazo ya jamii hurithishwa kizazi kimoja na kingine. Kuwepo na mikakati ya matumizi ya lugha katika jamii ni jambo ambalo hujitokeza kama lililo muhimu na la lazima katika jamii yoyote ile ikiwemo ile ya Nakuru. Mwanajamii huzipata lugha kupitia kwa elimu na mwingiliano wa mhusika na wengine. Hivi ndivyo lugha mjini Nakuru, ikiwemo ile ya Sheng zilivyopatikana. Kuwepo kwa matumizi ya Sheng katika mazingira ya mjini, shuleni, nyumbani na hata mazingira rasmi mjini Nakuru kunafanya iwe muhimu kuitafiti mada hii.

**1.6 Upeo na mikakati ya utafiti.**

Utafiti huu uliazimia kuchunguza namna lugha vipindi Sheng inatumika miongoni mwa wakaaji wa mji wa Nakuru, kwa kuegemea hasa majukumu yake na hata hadhi ya lugha hii. Sababu ya kuteua mji wa Nakuru ni kuwa Nakuru inapatikana katikati mwa miji yote ya Kenya na pia kwa sababu kuna wakaaji wengi mjini Nakuru wanaoishabikia lugha ya Sheng. Watafitiwa walikuwa ni wanafunzi wa shule za upili 5 mjini Nakuru. Sababu ya kuteua vijana wa shule za upili ni kwa sababu wana ujuzi wa lugha vipindi haswa Sheng na pia wanauelewa wa maswala ya utandaridhi mbali na kuwa na uelewa wa lugha za kikoloni, kitaifa na lugha asilia za kiafrika. Sababu ya kufanya utafiti huu katika shule 5 na zipo shule nyingi mjini Nakuru ni kwa sababu zipo mjini na zinakaribiana na

wanafunzi walioko katika shule hizi ni wa makabila tofauti na matabaka tofauti hivyo kuwakilisha matabaka na makabila yote nchini Kenya. Pia shule za upili zimekaribiana kwa hivyo kurahisisha gharama ya utafiti kifedha na hata kiwakati.

## 1.7 Msingi wa nadharia

Mada yetu ya utafiti inahusu hali, hadhi na majukumu ya Sheng mjini Nakuru, suala linalofungamana na matumizi ya Sheng katika jamii.

Utafiti huu umetumia nadharia ya lugha na utambulisho wa jamii ya Gumperz na Cook (1982), nadharia ya chanzo cha ujifunzaji wa lugha ya pili ya Krashen (1989) na nadharia ya jumuishi na utambulisho iliyoasisiwa na Gile (1979).

### **1.7.**1, **Nadharia ya lugha na utambulisho wa jamii.**

Nadharia hii iliasisiwa na Gumperz na Cook (1982) ambapo walieleza mwingiliano wa kimawasiliano na vikundi mbalimbali vya jamii ya kisasa.

Walitaka kuangazia mwingiliano wa binadamu ambao huleta jukumu la kimawasiliano wakitumia mtazamo wa isimujamii. Mtazamo huu huthibiti na kuzalisha kitambulisho cha jamii fulani. Wanaeleza kuwa huwa tunachukua jinsia, kabila na tabaka kama vithibiti au mipaka ya kuunda vitambulisho vyetu vya kijamii. Nadharia hii ilitusaidia kuangazia mwingiliano wa vijana katika jamii na jinsi vijana mjini Nakuru wanatumia Sheng kama kitambulisao lugha chao.

Ingawa katika lugha vithibiti hivi vya jinsia, kabila na tabaka huenda vikabadilika, tunapaswa kuelewa kuwa vithibiti hivi vina uhusiano na vitambulisho lugha na vinagusa jamii na jinsi uendeleaji wa mawasiliano huchipuka. Kwa mujibu wa nadharia hii lazima mawasiliano yaeleze jinsi yanavyomgusa binadamu na maisha yake. Kwa hiyo katika mawasiliano miongoni mwa vijana nadharia hii ilitusaidia kutambua jinsi Sheng inavyogusa vijana na maisha yao na jinsi vijana mjini Nakuru wanavyotumia Sheng kama kitambulisho lugha chao.

Jinsi vikundi mbalimbali vinavyoingiliana huleta tofauti kati ya maisha ya mijini; miji ya kisasa na ya hapo awali, na vile ambavyo watu binafsi wanavyoingiliana na sheria zinazowaongoza ni tofauti. Sheria zinazowaongoza vijana katika matumizi ya Sheng ni umri wao na pia maeneo wanayotoka vijana hawa.

Uasilia wa umoja wa jamii, ambapo familia ziliishi pamoja na zilizungukwa na ukabila au tabaka moja kwa sasa hautiliwi maanani haswa katika miji. Katika maisha yetu ya kila siku tunaendelea kujitegemea na kuingiliana na wale ambao tunaweza kushiriakiana nao kiutamaduni. Kutokana na kauli hii vijana mjini Nakuru wametoka katika mazingira tofauti na mwingiliano wao ndio huwawezesha kushirikiana na kuuendeleza utamaduni wao.

Kitambulisho cha jamii na kabila husababishwa na huhifadhiwa katika lugha. Kitambulisho cha jamii ya vijana mjini Nakuru kimehifadhiwa katika lugha yao ambayo ni Sheng.

Gumperz na Cook (1982) wanaeleza juu ya ukabila wa kikale na ule wa kisasa wakigusia mambo ya mawasiliano. Wanaeleza kuwa ukabila wa kisasa hujumulisha maeneo mbalimbali na matabaka mbalimbali. Ingawa mwanzoni mwa maingiliano huwa pana tofauti ya kimawasiliano kwa sababu ya tofauti zilizoko kati ya watu binafsi katika kabila hii wahusika hubuni lugha ambayo huleta uelewano kimawasiliano. Vijana mjini Nakuru hutoka kwenye maeneo tofauti tofauti na makabila tofauti lakini maisha mjini huwaunganisha hasa katika hali ya mawasiliano na uelewano wao hutokana na matumizi ya lugha yao ya jamii ambayo ni Sheng.

Nadharia hii ilitusaidia katika kazi yetu kwa sababu vijana wengi kutoka mji wa Nakuru hutoka katika maeneo tofauti tofauti, katika kabila tofauti na matabaka tofauti lakini huwa na kitambulisho chao cha kijamii ambacho ni lugha inayowaunganisha katika maisha yao ya mjini na ni Sheng. Lugha hii huwa na majukumu mengi miongoni mwa vijana katika kuendeleza maisha yao ya kila siku kwani ndiyo wanayoitumia sana.

Kitambulisho na maisha haswa ya vijana mjini yamehifadhiwa katika Sheng. Vijana wa umri wa miaka 14 na kuendelea hutaka kuhusishwa na vikundi fulani vya kijamii na ni lazima kila mmoja atoshee katika kundi hilo. Makundi hayo huundwa kulingana na matabaka, makabila na jinsia. Hivi ni vithibiti ambavyo Gumperz na Cook wanaeleza kuwa huunda vitambulisho vya jamii. Kama wahusika wametoka katika matabaka tofauti au makabila tofauti, lazima wawe na uelewano wa lugha na hapo lugha ya Sheng huchipuka. Nadharia hii ilitusaidia kuelewa, kutambua na kuipa nafasi jamii ya vijana mjini Nakuru na lugha yao.

**1.7.2. Nadharia ya chanzo cha ujifunzaji wa lugha ya pili.**

Krashen (1987) anaeleza kuwa katika kujifunza lugha ya pili haihitaji mhusika kuelewa au kujua kanuni za kisarufi bali anahitaji mwingiliano wake na watu wengine ili apate lugha ya pili, yaani ujifunzaji asili. Msemaji na msikilizaji hawajihusishi katika matamshi bali katika ujumbe unaowasilishwa na uelewa wao. Krashen anashughulikia ujifunzaji wa lugha na maendeleo yake.

Katika nadharia hii alijitokeza na haipothesia tano ambazo anaeleza juu ya ujifunzaji na uhifadhi wa lugha ya pili.

- Haipothesia ya upataji lugha kwa kujifunza .
- Haipothesia ya uzoefu wa matumizi ya lugha.
- Haipothesia ya kupata lugha kwa utaratibu asilia.
- Haipothesia ya upataji lugha.
- Haipothesia ya kuhifadhi au kuchuja lugha.

Haipothesia ya upataji wa lugha kupitia mafunzo ndiyo ambayo, Krashen anaiona kuwa ya msingi zaidi kuliko haipothesia nyingine zote na ambayo ilitumiwa sana na wanaisiimu. Kulingana na Krashen, kuna aina mbili za taratibu katika utekelezaji wa lugha ya pili.

Kuna utaratibu wa upataji na utaratibu wa kujifunza. Utaratibu wa upataji lugha hutokana na kuipata lugha kwa njia isiyodhihirika; kwa mfano jinsi watoto wapatavyo lugha yao ya

kwanza. Upataji huu huhitaji tu mwingiliano wa mhusika na jamii ndipo mtu apate lugha. Mhusika hujihusisha sana na tendo la mawasiliano.

Katika utaratibu wa mafunzo, lugha hupatikana kwa njia inayodhihirika yaani, mhusika hupata lugha kwa kusudi au kwa ufahamu wake. Kwa mfano, kupata lugha kwa kufuata sheria za kisarufi. Kulingana na Krashen upataji lugha kwa njia isiyodhihirika ni muhimu zaidi kuliko kupata lugha kwa njia ya mafunzo. Mjini Nakuru vijana wamepata lugha ya Sheng kwa njia inayodhihirika kwa sababu wao huipata kwa utaratibu na kwa kusudi au kwa ufahamu wao. Hata hivyo kuna jamii ya vijana wa kisasa ambao huongea na wanao Sheng kwa hivyo kizazi hiki huenda kikapata lugha ya Sheng kwa njia isiyodhihirika yaani jinsi watoto wapatavyo lugha yao ya kwanza.

Kwa mfano wengi wa madereva na utingo mjini Nakuru hutumia Sheng katika mazingira yao ya kikazi na hata nyumbani, huenda wanatumia lugha hii kwa wanao kwa hivyo kuwarithisha lugha hii. Ni kutokana na mwingiliano wa wahusika na wengine ambapo wao hujifunza lugha hii ya Sheng.

Katika haipothesia ya uzoefu wa matumizi ya lugha, Krashen anaeleza kuwa ni uhusiano ulioko kati ya upataji lugha na ujifunzaji lugha. Kulingana na Krashen utaratibu wa upataji lugha hutokana na matamshi na utaratibu wa mafunzo huchangia katika kumpa mtu uzoefu wa kupata lugha. Vijana mjini Nakuru wameishabikia Sheng na kutaka kuitumia sana kumepelekea wao kuwa na uzoefu wakuitumia katika mazingira ya mjini, nyumbani, hata shuleni.

Ujifunzaji wa lugha kwa ufahamu huwa kizuizi katika upataji wa lugha ya pili. Krashen anaeleza kuwa ili mtu awe na lugha hiyo ya pili, lazima awe na muda wa kutosha wa kujifunza, awe na ufasaha katika usemaji na msemaji atambue kanuni na sheria za kisarufi katika lugha ya pili. Hata hivyo, haipothesia hii ina dosari kwani msemaji huenda awe hakufunzwa sheria na kanuni zinazofuatwa katika matumizi ya lugha fulani au akafunzwa kwa njia ambayo haijafaa. Watu tofauti hutofautiana katika uelewa na utumizi wao wa lugha. Sheng ni lugha ambayo haijasanifishwa na inaonekana kama isiyo imara kwa hivyo haifuati kanuni na sheria za lugha.

Haipothesia ya kupata lugha kwa utaratibu asilia kwa mujibu wa Krashen (1987) ilitokana na utafiti uliofanywa na Dulay na Burt (1974); Fathman (1975); na Makino (1980). Haipothesia hii inaeleza kuwa upataji wa sarufi hufuata kanuni ambazo hubashiriwa. Kanuni zingine hupatikana mapema na zingine baadaye maishani lakini hutokana na uwazi au mwingiliano wa mhusika na jamii. Sheng ni lugha inayokuwa na inayoongeza misamiati kila uchao lakini maneno mengine hayatumiki kwa uwazi kwani hutumika ili kuhifadhi siri za wahusika.

Kuhusu haipothesia ya upataji lugha ya pili, Krashen anasema kuwa juhudi za upataji lugha ni uelewa wa lugha hiyo bali si utumizi wa lugha hiyo, matokeo yake huwa ni hali ya kuweza kuiandika na kuisoma. Haipothesia hii hujishughulisha na upataji lugha pasipo kujifunza. Haipothesia hii kwa kiasi inahitilafiana na kazi yetu kwa sababu juhudi za vijana mjini Nakuru si uelewa sana wa Sheng lakini matumizi yake ndiyo

wanashughulikia sana. Katika kuitumia Sheng wao hujisikia wakiwa sehemu muhimu ya jamii ya vijana.

Haipothesia ya mwisho ni ya kuhifadhi au kutupilia mbali lugha fulani; ambapo Krashen anaona kuwa mambo kadhaa huchangia katika kuihifadhi au kuitupilia mbali lugha fulani. Ili kuwa katika hali nzuri ya kupata lugha na kuihifadhi, mambo yafuatayo huchangia: kutokuwa na wasiwasi katika matumizi ya lugha, kujiamini na kujitia motisha. Mwelekeo chanya katika matumizi ya lugha fulani ni muhimu ilikuweza kuipata vilivyo na pia kuitumia. Vijana wengi mjini Nakuru wanajiamini sana wakati wanapoitumia lugha ya Sheng. Pia hujisikia wakiwa sehemu ya jamii na kama wanaokubalika na wenzao wakati wanaitumia. Hali hii imechangia katika kuhifadhiwa kwa Sheng miongoni mwa vijana.

Sababu ya kutumia nadharia hii ni kuwa kila msemaji lazima aipate lugha ili aweze kuwasiliana kwayo na wengine. Msemaji huzipata lugha tofauti tofauti katika nyakati tofauti na kwa njia tofauti tofauti na hivyo basi, lugha hizi hupata majukumu tofauti na huwa na hadhi tofauti kutegemea umuhimu wa lugha husika kwa wahusika. Pia utafiti huu ulihusu matumizi ya lugha zaidi ya moja kwa sababu kuna ulinganisho wa Sheng na lugha nyingine. Ujifunzaji wa lugha ya pili na jinsi mhusika anavyoipata huchangia sana katika majukumu, hali na hadhi ya lugha husika. Kama lugha nyingine yoyote ile ya pili vijana hupata Sheng kwa njia ya kujifunza ingawa ujifunzaji huu hutokana na mwingiliano wa mhusika na wengine.

### 1.7.3. Nadharia ya jumuishi ya utambulisho

Nadharia jumuishi ya utambulisho iliasisiwa na Gile (1979). Kimsingi nadharia jumuishi ya utambulisho inashughulikia uhusiano baina ya lugha na utambulisho wa mtu, jamii, jumuiya ama hata taifa kwa jumla.

Katika nadharia hii, Giles anaeleza kuwa utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi, lakini lugha hutumika katika mchakato huu kama ishara muhimu ya kueleza utambulisho huo husika, na jamii lugha inajengwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamiilugha moja ambayo iko tofauti na jamiilugha nyingine (Giles, 1979:253). Wakichangia dhana hii ya utambulisho Le Page na Tabouret-Keller (1989) wanasisitiza kuwa, ili utambulisho huu udumu, wanajamiilugha wenyewe wanastahili kuthamini na kudumisha kwa vitendo lugha yao pamoja na vibainishi vingine vya msingi vinavyowatambulisha.

Maoni haya yanatanuliwa na Little John na Foss (2008) wanaposema kwamba kama wazungumzaji wa jamiilugha fulani hawatakuwa tayari kudumisha utamaduni na lugha yao ya aisli iliyobeba amali za jamii yao, kuna kila dalili ya kwamba utambulisho wa jamiilugha hiyo unaweza kupotea (TY).

Nadharia hii ilitusaidia katika kubainisha umuhimu wa kufanikisha matumizi ya Sheng mjini Nakuru na kutambua Sheng kama kitambulisho cha vijana na kutofautisha Sheng na jamiilugha nyingine. Iwapo kudumisha utambulisho wa jamii ya vijana unatokana na

vitendo vya kuthamini lugha yao ya Sheng kama inavyoeleza nadharia hii, basi kutambua hali, hadhi na majukumu ya Sheng kutadumisha utambulisho wa vijana na wala hautapotea. Tunapozingatia lugha katika mawasiliano, lugha ya jamii inakuwa nyenzo kuu inayowasilisha hisia na mitazamo ya ndani, hivyo kufanya jamii kufasili mambo yote mbalimbali kwa njia tofauti na jamii nyingine. Kwa njia hii lugha inakuwa msingi wa maendeleo ya jamii yake (Msanjila na wengine, 2009:64) ambayo pia yanakuwa kibainishi cha utambulisho wa jamii husika.

## 1.8. Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti

Kazi zilizowahi kuandikwa juu ya Sheng ni nyingi, hata hivyo asilimia kubwa ziliiegemea isimujamii ambayo pia utafiti huu uliegemea.

Osinde (1986) alizungumzia Sheng kama lugha ya vijana, Abdulaziz na Osinde (1997), nao wanatazama Sheng kama msimbo mchananganyiko unaotumiwa na vijana katika miji ya kenya. Maoni kama haya yanaungwa mkono na waandishi wengine kama Spyropoulos (1987), Kembo-sure (1992).

Mazrui (1995) anasema kwamba Sheng ni lugha msimu wa vijana na kwamba lugha hii imejikita katika ubadilishanaji msimbo. Mazrui anazidi kusema kwamba faridi zilizokopwa kutoka Kiswahili na Kiingereza kwa kiwango kikubwa huhifadhi sifa zao za kiasili, Mazrui (1995:175). Maoni haya ya Mazrui yanatusaidia katika kueleza hali ya Sheng kimuundo.

Bosire (2006) anadai kwamba Sheng ni lugha chotara. Anasema kwamba, vijana ambao ndio watumizi wa lugha hii wamejikita katika mapisi fulani na hivyo wanatafuta njia za

kuasi mpangilio wa kijamii hasa mipangilio iliyoweka wanajamii katika ngazi tofauti tofauti kiuchumi, kihadhi na kimaeneo, njia moja wapo ya kuasi huku ni kutumia lugha inayopinga hali hizo kuwa katika usawa lakini kwa kufanya hivyo vijana hawa wamejikita kujitenga na wanajamii. Utafiti huu unatofautiana na mawazo ya Bosire, kwa sababu katika lugha yoyote ile wahusika tofauti hutumia lugha tofauti na si eti kwa sababu wanataka kujitenga na jamii lakini kusudi lao ni wayahifadhi au wayaweke siri mambo mengine ambayo hawataki yaeleweke na wahusika wasiokusudiwa. Maoni haya ya Bosire yanakaribiana na yale ya wanaodai Sheng ni msimbo wa siri unaotumiwa na vijana kuhifadhi siri zao miongoni mwao. Kuhifadhi siri zao hakumaanishi kujitenga na jamii. Kama vile ambavyo jamii nzima huhifadhi siri zao katika lugha pia vijana huhifadhi siri zao katika lugha yao ambayo ni Sheng.

Karanja (2010), anasema kwamba upekee wa Sheng upo katika uamilifu wake miongoni mwa watumizi wake. Karanja (2010:20), anazidi kusema kwamba masuala yaliyopelekea kubuniwa kwa Sheng ni yale yasiyokuwa ya kiisimu kwa sababu kulikuwa na lingua franka ambayo ingeweza kutumika miongoni mwa vijana. Lingua franka hiyo ni lugha ya Kiswahili. Sheng ni lugha ambayo imekopa maneno yake kutoka kwa lugha nyingine ingawa imejikita sana katika lugha ya Kiswahili hata hivyo kama yalivyo maoni ya Karanja tunaishughulikia kama lugha binafsi kihadhi na kimajukumu mbali na muudo wake.

Mukhwana (2008:150) anasema kwamba Sheng na Engsh ni lugha zenye umaarufu sana katika shule za Kenya. Huku akirejelea utafiti wake alioufanya Nairobi, Mombasa na Kisumu, Mukhwana anasema kwamba wazungumzaji wa lugha hizo hawawezi kujieleza kisahihi kwa Kiswahili au Kiingereza. Mukhwana anazidi kusema kwamba Sheng haina

kanuni za sarufi zilizo za lazima. Hivyo neno halina maana mahsusi na kwamba muhimu ni uelewano baina ya wazungumzaji na msilizaji. Aidha kilicho muhimu katika Sheng na Engsh ni usahili wa mawasiliano. Mtaalamu huyu ambaye amejikita katika isimujamii aneleza kwamba kama ilivyo katika Engsh, Sheng ni lugha iliyojikita katika muktadha. Anachosema Mukhwana ni kwamba muktadha ni kitu muhimu sana katika kufaulisha uelewano baina ya watumizi wa lugha ya Sheng. Kwamba muktadha ukiondolewa huenda pi maana ya neno ikabadilika. Kazi hii ya Mukhwana inatusaidia katika kueleza jinsi lugha ya Sheng hutofautiana kimatumizi na kimuktadha katika maeneo ambayo lugha hii inatumika.

Mbaabu na Nzuga (2008) wanasema kwamba Sheng ni lugha ya mjini iliyo na sintaksia kama ile ya Kiswahili na fonolojia yake vilevile inafanana na ya Kiswahili. Maoni haya si tofauti sana na yale ya Webb na Kembo-sure (2000:37), hasa wanapofananisha Sheng na pijini. Tujuavyo ni kwamba lugha moja ambapo ndiyo huwa msingi hutawala muundo wa pijini hivyo wataalamu wengi hukubaliana kwamba Sheng imebeba sifa za kimuundo za Kiswahili. Hata hivyo kuna lahaja za Sheng kulingana na mahali ambapo Sheng inatumika. Kwa mfano Sheng inayotumika Nyeri itakuwa na mchanyiko wa maneno ya Kikikuyu na ile inayotumika mjini Kisumu itakuwa na mchanyiko wa maneno ya Kidholuo. Ingawa lugha kuu katika kuunda Sheng ni lugha ya Kiswahili.

Githinji (2006b), amepiga hatua sana katika kujadili ubadilifu wa leskimu za Sheng. Madai yake ya kwamba Sheng inabadilikabadilika hasa katika kiwango cha msamiati ni madai ya kuangaliwa kwa jicho pevu. Tunaonelea kwamba kusema kuwa msamiati fulani unabadilika na hautumiki tena si kigezo bora cha kudai kwamba lugha fulani ni badilifubadilifu. Kufifia au kufa kwa msamiati huenda ni hali ya kawaida ya lugha ya

kudhihirisha ukuaji wake au hata uimalikaji wake jambo ambalo utafiti huu unachunguza kwa kuonyesha jinsi Sheng inavyoongeza misamiati yake na jinsi misamiati tofauti inavyotofautiana kimatumizi katika maeneo tofauti.

Momanyi (2009), anaelekea kulaumu Sheng katika matumizi mabaya ya Kiswahili, kwamba Sheng imekuwa na athari kubwa sana katika kukichafua Kiswahili. Haya ni maoni ya wengi wakiwemo waandishi wa habari na walimu wa shule za upili. Swali linalotujia ni kwamba, je, Kiswahili kisosanifu ni Sheng? Jibu la swali hili haliwezi kupatikana katika utafiti huu maana kufanya hivyo tutaondoka mipaka na upeo wa kazi hii. Hata hivyo matumizi ya lugha yoyote ile haswa matumizi ya lugha ya kwanza huathiri matumizi ya lugha ya pili. Huenda lugha ya pili ikaathiriwa kimatamshi, kisarufi au hata kimaandishi.

Kazi nyingi sana zimeandikwa kuhusu Sheng kuna wataalamu walioshughulikia lugha msingi ya kubuniwa kwa leksimu za Sheng kama vile Mazrui na Mphande (1990), Githiora (2002), Ogechi (2005) na Warambo (2011). Wataalamu hawa wameelekea kukubaliana kwamba lugha msingi ya uundaji wa leksimu za Sheng ni Kiswahili. Wanasema kwamba sarufi ya Sheng inaoana na ile ya Kiswahili. Ingawa lengo la utafiti huu si kuchunguza kubuniwa kwa leksimu za Sheng. Madai ya wataalamu hawa kuhusu ushabiliano wa kisarufi baina ya Kiswahili na Sheng yatatusaidia kubainisha hali kwa wakati huu, hadhi ya Sheng na maendeleo ya Sheng kama lugha inayotumika katika mijini mingi nchini Kenya kukiwemo haswa mji wa Nakuru.

Lugha imefinyangwa kwa njia tofauti ili kutumiwa kama kifaa cha kupitishia ujumbe kuhusiana na maswala tofauti tofauti ya kijamii. Wakati tunapotumia lugha tunafanya hivyo kama watu binafsi walio na historia za jamii husika.

Edward, J (2009) anaeleza juu ya lugha kama kitambulisho, cha mtu binafsi na kikundi cha watumizi lugha katika jamii. Anasema historia yetu hueleza uhusiano wetu katika vikundi vya kijamii tulivyozaliwa; vyaweza kuwa vikundi vya kijinsia, kijamii, kitabaka, kidini, kimaeneo au kitaifa. Mambo haya ya kijamii hujenga vikundi mbalimbali tunavyojiunga navyo pamoja na mitazamo ya kimaadili, imani, itikadi na hisia zinazohusiana na vikundi hivi. Pia mambo haya huchangia katika ukuaji wa vitambulisho vya kijamii kama vile huchangia katika jukumu la uzungumzaji na elimu ya lugha husika. Kwa hiyo Sheng ni kitambulisho lugha ambacho kinaelezea historia ya vijana hasa wa mjini Nakuru ambao ni sehemu muhimu katika jamii. Vijana wanatumia Sheng kueleza hisia zao, mitazamo yao ya maadili, imani na itikadi zinazohusiana na vikundi vyao mjini Nakuru.

Hanks (1996:201) anasema kuwa katika tajriba yetu tunatumia lugha si kama mtu binafsi kwa kutoa sauti tu ili kukidhi mambo yetu binafsi lakini katika nyanja za kijamii ambazo huchukua nafasi na huendanisha na kila mmoja wetu katika jamii.
Kwake Hanks (ibid), tuna uwezo wa kujiunga na vikundi mbalimbali katika jamii kwa kujihusisha na mambo yanayohusiana na jamii kama vile shule, kanisa, familia na hata kazi. Kwa hiyo vijana wanapotumia Sheng kama kitambulisho lugha chao ni njia moja wapo ya kujiunga na kujihusisha na kikundi fulani katika jamii. Mambo yao yanahusiana

na maisha ya kila siku huweza kuelezwa kwa kutumia Sheng. Ni katika vikundi vyao ambapo wanajisikia wametosheka na kujisikia kama sehemu ya jamii na hujihusisha na mambo ya kijamii katika vikundi hivi.

Hudson (1995) aliutafiti ushirikiano uliopo baina ya lugha na jamii na akaibua hoja kuwa kuna njia tofauti ambazo kwazo makundi tofauti ya jamii hutumia lugha. Msomi huyu aliibua fikra kuwa lugha kama inavyotumika na makundi tofauti ya kitabaka hubadilika kama vile hali zao zinavyobadilika kitabaka. Anasema bayana kuwa wafanyakazi katika sehemu tofauti tofauti hutumia lugha kwa njia iliyo tofauti.

Utafiti wetu ulilenga haswa matumizi ya lugha vipindi Sheng miongoni mwa jamii na makundi tofauti tofauti ya watu mjini Nakuru. Utafiti huu ulitarajia kubainisha hasa jinsi Sheng inavyotumiwa katika nyanja tofauti za maisha huku hadhi na majukumu yake yakionyeshwa. Kwa hiyo kama vile kunavyo njia tofauti ambazo kwazo makundi tofauti ya jamii hutumia lugha, ndivyo kama vile kunavyo kuwa na njia tofauti ambazo kwazo makundi tofauti ya jamii hutumia lugha, na ndivyo ambavyo vijana kama sehemu ya jamii wanavyotumia lugha yao ya Sheng. Sheng pia huenda ikabadilika kimatumizi katika maeneo tofauti mjini Nakuru kulingana na matabaka yaliyoko mjini Nakuru.

Trudgill (1983:100) anasema kuwa katika jamii nyingi, usemi wa wanaume na wanawake hutofautiana. Anashahidia kauli hii kwa kusema kuwa lugha haitofautiani tu kuambatana na tabaka la kijamii, kikundi cha kikabila, umri na jinsia ya msemaji lakini vilevile muktadha wa hali huchangia. Lugha vipindi kama vile Sheng hutumika sana miongoni

mwa vijana ili kukidhi mahitaji yao ya kimawasiliano haswa ya kisiri. Kulingana na utafiti huu nilielezea katika sura ya nne jinsi matumizi ya Sheng yanavyotofautiana kijinsia kwa hiyo wazo hili la Trudgill litatusaidia katika kutambua utofauti wa matumizi ya Sheng kijinsia.

Trudgill (1983:13) anasema kuwa lugha haimaanishi kupitisha ujumbe tu, lakini pia ni muhimu katika kujenga uhusiano. Matumizi ya lugha tofauti tofauti huweza kuelezea na pia kubainisha uhusiano ulioko kati ya wahusika. Matumizi ya Sheng haimaanishi kupitisha ujumbe miongoni mwa vijana pekee lakini pia kujenga na kuboresha uhusiano wao. Sheng hueleza uhusiano baina ya vijana wakiwa pamoja na matumizi ya lugha nyinginezo kama Kiswahili na Kiingereza pia hueleza uhusiano ulioko baina ya wahusika kwani hutumiaka katika miktadha tofauti tofauti.

### 1.9. Mbinu za utafiti

Sehemu hii ilihusika na uteuzi wa watafitiwa, utaratibu wa ukusanyaji wa data, vifaa vya ukusanyiaji data na uchanganuzi wa data yenyewe.

### 1.10. Uteuzi wa watafitiwa

Data ilichukuliwa kwa kuchagua kimaksudi watafitiwa ambao ni wa shule za sekondari katika eneo la mji wa Nakuru waliteuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Wanafunzi 60 kutoka kwa shule za sekondari 5 kila shule ikiwa na watafitiwa 12 katika mji wa Nakuru. Watafitiwa walikuwa watumizi wa lugha tofauti haswa za kimataifa, kitaifa, kiasilia na

Sheng. Lengo la kuwachagua wanafunzi wa sekondari ni kwa sababu wana uelewa wa lugha tofauti na ndio vijana wanaotumia na kuishabikia Sheng sana.

### 1.11. Ukusanyaji wa data

Mtafiti alitaraji kutumia njia tofauti kukusanyia data ambazo zilihusiana na utafiti wake. Mbinu za ukusanyiaji wa data zilihusisha utumizi wa hojaji ambapo watafitiwa walitakiwa kutumia lugha ya usemi halisi katika kuzijaza hojaji. Baada ya hojaji za kwanza kujazwa, mtafiti alijua jinsi ya kuwaelekeza watafitiwa ikiwa walikuwa na ugumu. Pia palikuwa na maswali ya moja kwa moja ikiwa maswali yaliyo kwenye hojaji hayakueleweka kwa ufasaha.

### 1.12. Vifaa vya ukusanyaji wa data

Kifaa kilichotumia ni hojaji; pia kuhitimika karatasi ya maswali ya uchunguzi.

### 1.13. Uchunganuzi wa data

Nilichanganua data kwa kutumia mbinu ya maelezo; hii ilipatika baada ya kuangalia namna watafitiwa walivyokuwa wamejielezea kwenye hojaji. Matokeo yetu yalitolewa kwa kuegemea matokeo kulingana na asilimia katika majibu kwa maswali yetu.

# SURA YA PILI

# LUGHA ZINAZOTUMIWA MJINI NAKURU

## 2.0. Utangulizi

Lugha ni kifaa muhimu situ kama njia ya kuwasilisha mawazo, lakini pia katika kuujenga urafiki na utangamano wa kitamaduni na kiuchumi katika jamii. Katika historia yote ya mwanadamu, watu wengi wameangazia umuhimu wa lugha. Lugha huelekeza mawazo na hisia kwa kubainisha kwa yakini mtazamo wa watu. Lugha hutokea kutumiwa kwa njia tofauti tofauti ili kufanikisha mawasiliano. Matumizi, majukumu na hadhi ya lugha hutegemea sana mazingira ambamo lugha inatumika.

Sura hii ina dhamira ya kuangazia lugha zinazotumika mjini Nakuru ambazo ni Kiingereza, Kiswahili, lugha asili za Kiafrika na lugha vipindi za Sheng na Engsh ili hali hii iwe kama msingi wa yale tutakayojadili baadaye katika kazi hii.

## 2.1. Lugha ya Kiingereza

Nyakati za ukoloni, kulikuwa na ugumu wa kuunda sera ya lugha muhimu katika kutekeleza majukumu muhimu hasa ya kiserikali. Nchi ya Kenya ilitawaliwa na Mwingereza. Baada ya Mwingereza kuondoka lugha ya Kiingereza ilipewa ufahari na hadhi ya juu hivyo ikawa lugha rasmi ya kwanza na ya kimataifa. Lugha ya kiingereza ilitumika na pia sasa hutumika katika nyanja mbalimbali kama vile; nyanja za kielimu, kiuchumi, mahakamani, hutumiwa bungeni na pia kazi nyingi rasmi huandikwa kwa kutumia lugha hii ya Kiingereza. Pia Kiingereza ni lugha ambayo hutumika katika

mawasiliano na maingiliano ya kitaifa, Kenya. Inachukuliwa kama lugha iliyo kuu na muhimu kwa wakenya wote.

Kiingereza hutekeleza majukumu ya kimataifa hasa katika mawanda ya siasa, mikataba ya kimataifa na ni muhimu zaidi katika sayansi na teknolojia. Kiingereza ndiyo lugha inayotumika katika kuwasiliana kuhusu vipengele vingi zaidi vya tamaduni za ulimwenguni kote.

Kiingereza ni lugha ambayo ina umuhimu mkubwa zaidi kielimu dhidi ya lugha nyingine nchini Kenya kwa sababu ina vifaa vingi vya kufunziwa na kusomewa na hivyo elimu mara nyingi inaendeshwa kwa lugha hii.

Kupitia kwa Kiingereza watu kutoka maeneo tofauti tofauti duniani wanapata tajriba sawa na zile za watu waliostawi zaidi kiutamaduni. Inawafanya watu kutoka katika utamaduni mmoja kupata na kupanua utamaduni wao kupitia kwa utamaduni mpana wa lugha ya kimataifa. Kiingereza ni chombo cha kuendeleza na kuustawisha utamaduni wa kimataifa miongoni mwa mataifa ya ulimwenguni kote kukiwemo Kenya.

Mji wa Nakuru huwa na wakaaji wengi ambao wametoka katika maeneo mbalimbali nchini Kenya na pia wengine ambao wametoka katika nchi nyingine za Afrika. Wakaaji wa Nakuru haswa wale wa tabaka la juu huitumia lugha ya Kiingereza katika mawasiliano yao ya kila siku na hutamani pia watoto wao wawasiliane kwayo. Ni lugha

ambayo pia hutumika kwenye televisheni na redioni. Ingawa lugha ya Kiingereza ndiyo inayo sifa kuu, lugha nyingine hutumika mjini Nakuru pia.

Tofauti na lugha ya Kiswahili ambayo huwa lugha ya taifa, lugha ya Kiingereza hutumiwa kama lugha ya kimataifa katika mji wa Nakuru. Inatekeleza majukumu ya kidiplomasia, biashara za kimataifa, na usafiri wa kimataifa. Kiingereza pia hutumika kama lugha unganishi katika masuala ya ubadilishanaji wa mambo ya kiutamaduni baina ya jamii nyingi mjini Nakuru. Mambo haya ya utamaduni yanahusu mambo kama vile vifaa vya ujenzi, utendakazi, utamaduni wa mazingira, utamaduni wa kijamii, utamaduni wa kidini na mpangilio wa kisiasa na kiutawala.

Mjini Nakuru Kiingereza ni lugha ambayo inatumika kuwaunganisha watu wanaoongea lugha ambazo hazijakua zaidi kiutamaduni kama nyingine. Lugha hizi mara nyingi huwa za watu wa mataifa ambayo hayajaendelea sana kiutamaduni. Pia ni lugha ambayo hutumiwa katika shughuli za utafiti na udenguzi mjini Nakuru hasa katika vyuo vikuu.

Kisheria lugha ya Kiingereza inatumika katika shughuli rasmi za kijamii nchini Kenya. Nchini Kenya na katika mji wa Nakuru lugha hii inatumiaka katika mianda rasmi ya bunge la taifa, la kaunti na la seneti, taaluma mbalimbali, afisini, elimu, salamu, teknolojia, warsha, kongamano, mihadhara na vikao vyovyote rasmi.  Kiingereza ni lugha ambayo hutumika sana kwenye vyombo vya habari.

Kwa mfano vipindi vingi vya televisheni hutumia lugha hii. Matangazo mengi ya kibiashara hutujia kupitia lugha ya Kiingereza.

Asilimia 100 ya watafitiwa kutoka shule za sekondari mjini Nakuru walisema wanaumilisi wa lugha ya Kiingereza. Hii ni kwa sababu Kiingereza ndiyo lugha ambayo inatumika katika nyanja za elimu. Ingawa lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi,wengi wa wakaaji wa Nakuru wanatumia lugha ya Kiingereza katika mazingira rasmi ikilinganishwa na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kulingana na hojaji zilizojazwa lugha ya Kiingereza inachukuliwa kama lugha ya watu walio na elimu ya ngazi ya juu na ni lugha inayohushishwa na wasomi (Tazama jedwali la pili). Pili pia Kiingereza ni lugha inayohusishwa na watu watabaka la juu na huhusishwa na "Wazungu'. Kwa sababu ni lugha ya mkoloni, lugha ya Kiingereza inachukuliwa kuwa ya kifahari na iliyo na hadhi ya juu mjini Nakuru.

**2.2. Lugha ya Kiswahili**

Kiswahili ni lugha ambayo inatambulika kama lugha ya taifa nchini Kenya. Lugha ya taifa ni ile iliyochukuliwa kutumika katika taifa zima na iliyoweza kutekeleza wajibu wa taifa. Lugha ya taifa inaweza kuwa kitambulisho cha utaifa na hufanya kazi ya kuunganisha wote walio katika taifa husika mathalau Kenya.

Nchi zilizo na wingilugha haziwezi kutumia lugha zote kutekeleza na kumudu shughuli zote za kitaifa na kwa hivyo huhitaji lugha ya taifa. Lugha ya taifa hunuiwa kuwa lugha itakayodumisha umoja wa kitaifa. Lugha hii hutekeleza jukumu la kitaifa katikanyanja

mbalimbali kama vile siasa, elimu na uchumi. Lugha ya taifa yaweza kuwa ni lugha ya kikabila, ya kijimbo au ya kigeni. Ni lazima lugha ta taifa iwe yenye matumizi mapana katika taifa husika. Katika nchi nyingi, hakuna tofauti katika matumizi ya lugha ya taifa na lugha rasmi.  Kwa mfano nchini Kenya lugha ya Kiswahili imepewa nafasi ya kuwa lugha ya taifa na pia lugha rasmi ya pili (Kiingereza kikiwa lugha rasmi ya kwanza).

Katika mji wa Nakuru lugha ya Kiswahili hupigania kuleta umoja wa taifa la Kenya kilugha. Maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kisayansi yanawezekana zaidi iwapo jamii imeungana kuliko kama imegawanyika. Mjini Nakuru haya huwezekana kupitia kwa lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili.

Watafitiwa mjini Nakuru walikubali kuwa Kiswahili ni lugha ya mjini na ya watu wote, yaani ya wazee kwa watoto na kwa vijana. Kiswahili huendeleza utamaduni sawa wa kitaifa na hivyo kuwaunganisha na kuwafananisha wakaaji wa Nakuru kama watu wa jamii moja.  Kiswahili huleta usawa miongoni mwa wazungumzaji wa lugha mbalimbali mjini Nakuru, pia husaidia katika harakati za uongozi kwa sababu ni vigumu kutawala kama eneo hili litagawika kikabila au kilugha na pia kurahisisha shughuli za serikali katika uongozi. Kiswahili huwaunganisha watu mjini Nakuruna ambao wametoka katika makabila namaeneo mbalimbali katika taifa la Kenya ili waweza kushirikiana na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya nchi ya Kenya. Lugha ya Kiswahili imeziba mipaka ya kikabila miongoni mwa wakaaji wa mji wa Nakuru.

Kiswahili ni lugha inayoonyesha uzalendo miongoni mwa wakaaji wa mji wa Nakuru ambapo kupitia kwa lugha hii wanaonyesha upendo na uzalendo wao kwa taifa la Kenya. Kiswahili ni kama kitambulisho cha uzalendo mjini Nakuru.

### 2.3. Lugha za Kienyeji

Lugha imeyafumbata maswala mengi ya jamii na utamaduni na kwa misingi hii itakuwa ni kukosa dira kwa mtu yeyote kuzungumzia lugha na kutokea kutouzungumzia utamaduni. Buliba na wenzake (2006:20) wanasema kwamba swala la lugha na utamaduni limetazamwa na wataalamu katika njia mbili: kwanza, kuna wanaochukulia lugha kama chombo muhimu cha kuelezea na kuendeleza utamaduni wa jamii yoyote ile. Pili, kuna wale ambao wanaiona lugha kama sehemu ya utamaduni.

Lugha ndiyo inayotuonyesha jamii ni nini na inaelezea watu wanaowasiliana wakitumia lugha hiyo. Imedokeza kuwa maisha ya jamii hupitishwa kwa mtoto kupitia kwa lugha. Kwa njia hii mtoto hujifunza utamaduni wa jamii yake, taifa, itikadi na mambo muhimu yanayothaminika na jamii yake. Jambo hili hufanikishwa kupitia kwa maingiliano yake na wenzake na kupitia kwa matumizi ya lugha ya kawaida akiwa nyumbani. Katika misingi hii itakuwa ni vigumu sana kuitenganisha lugha na utamaduni. Buliba na wenzake (ibid. 88) wanasema kuwa kuna mwingiliano mkubwa kati ya lugha, utamaduni na jamii.

Lugha hutumiwa na jamii kufafanua imani, itikadi, siasa, uchumi na mifumo yote ya jamii husika. Utamaduni ni mkusanyiko wa fikira na falsafa za watu, ada, desturi, mila,

siasa na uchumi. Kwa kawaida lugha huhusishwa na mazingira ambamo watu hao wanaishi. Mwingiliano wa jamii kwa kawaida hupeleka jamii moja kukopa dhana zingine ili kufidia upungufu ambao hudhihirika katika utamamaduni wao. Lugha kwa kawaida husaidia kudhibiti uhusiano wa kijamii, kwa kuwa lugha ndiyo inayowezesha watu kuwa na maingiliano yenye manufaa. Aidha, kuwepo kwa lugha kuna maanisha kuwepo kwa mtu anayekubalika na jamii yake. Jamii hujengwa na watu tofauti, na lugha ndiyo iwaletayo pamoja na kujenga uhusiano wa kibinafsi katika kiwango cha mtu na mtu, mtu na jamaa yake, na mtu na jamii zake katika shughuli zozote za kitamaduni.

Mjini Nakuru asilimia kubwa inayotumia lugha za kienyeji ni Wakikuyu, Wakalenjini (Wanandi na Wakipsigis), Dholuo, Wakisii, Waluyha na Wamaasai. Kuna makabila mengine mengi katika mji wa Nakuru. Jamii hizi hujihisisha na lugha zao haswa wakati wanawasiliana wenyewe kwa wenyewe. (Tazama jedwali la pili) utafiti huu ulionyesha kuwa lugha za kienyeji hutumiwa ili wahusika waweze kujihusisha na jamii au kabila lao. Ni lugha za kikabila ambazo ni kitambulisho cha mtumiaji lugha na kabila au aila yake. Lugha za kienyeji hutumiwa ilikuleta uhusiano mwema baina ya watu wa jamii au kabila moja na kwa hiyo, ni njia mojawapo ya kuhifadhi siri na tamaduni za jamii husika. Watu wakabila moja hutumia lugha hii ya kikabila katika maongezi yao ya kawaida, ya kisiasa na ya kibiashara mjini Nakuru.

### 2.4. Lugha Vipindi Sheng na Engsh

Kulingana na Ken Osinde (1990), Engsh ni lugha iliyokua mjini Nairobi sehemu ya Westlands; Kieslling na Moss (2004) na Nzunga (2000), wanaeleza kuwa Sheng ni lugha

inajumulisha maneno ya Kiingereza na pia hukopa maneno kutoka lugha ya Kiswahili na lugha asili za Kiafrika.

Githiora, C. (2000), anasema Sheng ni mchanganyiko wa lugha katika jamii au kikundi cha watu walio na wingilugha haswa kwenye miji mingi nchini Kenya. Sheng na Engsh ni lugha ambazo hutumiwa sana na vijana walio kati ya umri wa miaka 14 na kuendelea kama watafitiwa walivyoeleza. Sheng na Engsh ni lugha ambazo hutumika katika mazingira nje ya masomo darasani. Misingi ya sintaksia ya Engsh ni Kiingereza lakini pia hukopa maneno kutoka lugha nyingine. Msingi ya sintaksia ya Sheng ni Kiswahili lakini pia hukopa maneno kutoka lugha nyingine za asili ya Kiafrika ingawa haijikiti kwazo. Maneno kutoka lugha zingine hutoholewa na kuingizwa katika lugha hizi. Sheng na Engsh zinajulikana kama lugha za vijana haswa wa mijini nchini Kenya. Ni lugha ambazo zinahusishwa na watu wa umri fulani, tabaka na jinsia fulani. Katika utafiti wangu, wengi wa wanafunzi walitumia lugha hizi kuyajibu maswali yao haswa ya moja kwa moja.

(Tazama jedwali la pili) Sheng inatambulika kama lugha ya vijana na asilimia 84 ya vijana inatumia Sheng katika mawasiliano yao ya kawaida na huitumia kama kitambulisho chao kilugha. Ingawa Sheng na Engsh ni lugha ambazo hazijatambulikana kisheria, mjini Nakuru na nchini Kenya kwa ujumla, wengi hawazitumii kama lugha zao za kwanza lakini huzitumia katika miktadha fulani hasa katika majadiliano na mazungumzo ya vijana kwa vijana. Hii ni kumaanisha kuwa Sheng na Engsh hutumiwa sokoni, mitaani na pia nyumbani.

Sheng ni lugha ambayo inaendelea kukua kwani kwa wakati huu inatumika kwenye redio, televisheni na hata magazetini. Kwa mfano kuna *Ghetto redio* ambayo ni stesheni inayotumia Sheng kama lugha kuu, matangazo ya kibiashara yanaletwa kwa kutumia Sheng k.m tangazo la *(OLX)*, na vipindi vya televisheni kwa mfano kipindi cha *Machachari* katika stesheni ya *citizen* wahusika wengi ambao ni vijana na wanaowakilisha matabaka tofauti; walio wa tabaka la chini na waliotoka vitongoji duni huwasiliana kwa Sheng. K.m mhusika *Bahati* na *Ngovi wanawakilisha vijana waliotoka kwenye vitongoji duni na wanawasilana kwa Sheng hata hivyo wanawavutia hata vijana kutoka tabaka la juu k.m mhusika ambaye anawakilisha tabaka la juu.*

Tofauti kati ya Sheng na Engsh ni kuwa Sheng inahusishwa na vijana wa tabaka la chini ambao wametoka kwenye vitongoji duni na Engsh inahusishwa na vijana wa tabaka la juu. Ingawa Sheng inahusishwa na tabaka la chini ni lugha inayoendelea kukua, watumiaji wake kuongezeka na hata misamiati kuongezeka, (tazama jedwali la pili).

Katika utafiti wangu wengi wa vijana wa mitaani mjini Nakuru waliotafitiwa wanaitumia lugha ya Sheng kama kitambulisho chao. Hawa ni vijana walio kati ya miaka 14 na 20 na kwa kawaida hutumia Sheng ilikubana na kuficha mawasiliano yao haswa wakati hawataki wazazi au walimu wao kuelewa wanachokisema.

## 2.5. Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia lugha zinazotumika mjini Nakuru. Lugha tofauti tofauti hutumiwa na wahusika tofauti tofauti ili kukidhi mahitaji tofauti ya kijamii na ya kimawasiliano. Hivi ni kumaanisha kuwa lugha tofauti huwa na hali, hadhi na majukumu tofauti kulingana na watumizi wake na nafasi ya lugha katika taifa zima. Tofauti na hayo hali ya lugha fulani huipa lugha umuhimu wake na hata hadhi yake katika jamii husika. Lugha zote zina umuhimu kwani hujenga mahusiano ya mtu binafsi na jamii nzima na hata huendeleza jamii na nchi kwa ujumla.

Katika sura ifuatayo tutapiga hatua zaidi kwa kuangalia suala la hali, hadhi na majukumu ya Sheng mjini Nakuru.

# SURA YA TATU

# HALI, HADHI NA MAJUKUMU YA SHENG MJINI NAKURU

## 3.0 Utangulizi

Krashen (1987) anaeleza kuwa katika kujifunza lugha haihitaji mhusika kuelewa au kujua kanuni za kisarufi za lugha husika bali mhusika anahitaji mwingiliano wake na watu wengine ili apate kuijua lugha husika. Kwa hiyo katika kuelewa hali, hadhi na majukumu ya Sheng haihitaji kuelewa kanuni za kisarufi za lugha hii lakini jinsi vijana wanavyoingiliana kupata lugha hii.

## 3.1. Hali na hadhi ya Sheng

Ili kubainisha hali na hadhi ya Sheng kama lugha mjini Nakuru tunalazimika kuelezea hali ya isimujamii nchini Kenya kabla na baada ya ukoloni. Kabla ya ukoloni kila kabila nchini Kenya liliishi kivyake na mipaka ilionyesha wazi mazingira ya kabila fulani.Kila kabila lilihakikisha kuwa mila, tamaduni na imani yao ilihifadhiwa vilivyo. Makabila yalihakikisha kuwa mwingiliano wao na makabila mengine haungehasiri mila na tamaduni zao. Hivyo, maingiliano ya makabila tofauti nchini Kenya yalikuwa machache na yaliyodhibitiwa.

Wakati mkoloni aliingia nchini Kenya akawa kizuizi cha mipaka na majimbo ya makabila tofauti hivyo basi kuzuka kwa miji iliyowavutia Wakenya wengi kutoka makabila tofauti tofauti. Katika hali hii, mkoloni alisaidia katika kuwatenganisha Wakenya wa kabila moja kwa kuundwa kwa wilaya tofauti na katika wilaya hizi kukawa

na miji iliyojengwa. Kwa wakati huu nchi ya Kenya ina wilaya zaidi ya mia moja ambapo kila wilaya inazaidi ya wakaaji wa kabila moja. Hivi ni kumaanisha kuwa kunazaidi ya lugha za kiasilia na lahaja arubaini nchini Kenya. Lugha nchini Kenya zimegawanya watu katika kategoria tatu kuu ambazo ni Bantu ambapo takribani ya Wakenya asilimia 63 hutumia, Niloti asilimia 14 na Kushiti ni asilimia 3 ya Wakenya. Asilimia 2 iliyobakini hutokana na watumizi wa lugha nyingine za kigeni (Samper 2002).

Sababu ya watu kuhama kutoka maeneo yao asilia ni kutafuta kazi na katika mwingiliano huu pakawa na nafasi nzuri ya kuchanganya misimbo na hii ndiyo sababu kuu ya kuzuka kwa Sheng na Engsh nchini Kenya. Kando na lugha za kienyeji nchini Kenya kuna lugha za kigeni k.m (Vifaransa, Kijerumani, Kiitaliano) na Kiingereza ambayo ni lugha rasmi. Kiswahili ni lugha ya taifa na pia rasmi na hutumika sana na makabila tofauti tofauti. Lugha za kiasilia huonekana kama zilizo za hadhi ya chini na hupewa nafasi ya mwisho kihadhi (Abdulazizi 1972).

Baada ya ukoloni ni vigumu kupata mtu aliyeishi mjini nchini Kenya akiwa mwana umojalugha (Nzunga 2000). Samper (2002) anakubali, kuwa ni vigumu kupambanua karegoria ya Sheng kiisimu kwa sababu haijatambulika kama ni jagoni, au kama ni argoti, msimbo, kirioli, pijini au lugha vipindi, lakini inahusisha kila moja wapo wa haya na wakati mwingine kudhihirika kama ni mtindo fulani wa lugha katika jamii. Baadhi ya wataalamu hawa ni Bosire (2006:185), Aseka (1999), Spyropoulos (1987), Mazrui (1995), Osinde (1986) na Iribemwangi na Mukhwana (2011).

Sheng hubadilika kila uchao na kwa msingi huu huhusishwa na vijana na wengi huiona tu kama lugha isiyo na ufasaha.

### 3.1.1. Sheng kama lugha vipindi.

Hata hivyo katika kazi hii tunachukulia Sheng kama lugha vipindi. Kwa mujibu wa Iribemwangi na Mukhwana (2011) lugha vipindi hujulikana pia kama lugha msimu. Lugha hizi ni lugha vipindi au msimu kwa kuwa katika hali halisi, lugha zenyewe hazidumu bali hufifia au hujifia namna vipindi au misimu inavyobadilika kiwakati.

Kihistoria, lugha vipindi zilionekana kama lugha chafu. Pia, kihistoria matumizi ya lugha vipindi yalikuwani ya kuepuka au kuficha mambo yanayohusu mbeko na miko ya masuala ya kijamii kwa ujanja wa matumizi ya lugha. Inaaminika kuwa ni kutokana na hali hii ndio kwingi lugha vipindi hutumika zaidi katika masuala yasiyozungumziwa hadharani kama vile mapenzi, uhalifu na pia utumiaji na uuzaji wa dawa za kulevya.

Kwa misingi hii, lugha vipindi zinakuwa na msamiati maalum au wa kipekee na unaotumiwa na vikundi vya watu wenye sifa au tabia mbaya na zinazofanana. Pia, kwingi watumizi wa lugha vipindi huwa ni watu wa tabaka la chini na kwa hiyo lugha vipindi ni lugha duni na pia zisizo na adabu. Hivyo basi, kihisia na kimtazamo lugha vipindi ni lugha duni na zisizo na adabu wala mbeko na kwa hiyo ni lugha za viwango vya chini zikilinganishwa na lugha sanifu. Kimsamiati, lugha vipindi hujumuisha maneno mapya au maneno ya kawaida na yanayotumiwa kwa njia maalum na kwa namna spesheli.

Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa lugha vipindi hujitokeza pale ambapo watumizi wa lugha fulani hujitokeza na matumizi ya maneno au msamiati maalum usio rasmi ili kuelezea kitu au hali fulani kwa njia au namna isiyo ya kawaida. Lugha vipindi hazijali sheria za kisarufi na huzungumzia mambo au matukio ya kila siku katika jamii. Msamiati wa lugha vipindi hunuiwa kufasiriwa kwa urahisi hata kama si kwa njia ya moja kwa moja kwa kuwa maneno katika lugha vipindi hutumiwa kama isitiari.

Msamiati wa lugha vipindi huwa finyu na chakavu. Kwa hali, hii inakuwa ni lazima msamiati mwingine uongezewe, ule uliopo ufanyiwe juhudi za kuuundwa upya au ubadilishwe kwa maneno mapya na pia dhana mpya kila uchao.

Msamiati wa Sheng unajidhihirisha kama ulio mpanuzi kwa kubadilikabadilika. Kwa mfano maneno yafuatayo hutumika kwa maana moja ya gari: *nganya, ndae, buu, mathree*. Mfano huu unadhihirisha kuwa lugha vipindi huwa na uteuzi mpana wa msamiati.

Kama inavyoonekana kutokana na mifano hii, kuna wingi wa msamiati kwa dhana zile zile katika lugha vipindi. Hali hii hutokana na ukweli kuwa mara nyingi msamiati wa lugha vipindi huchakaa haraka na inabidi ubadilishwe kutegemea masiala mbalimbali kama vile uzoefu wa wahusika, nia ya mawasiliano, walengwa wa mawasiliano, tabaka la wahusika, mazingira ysa kimuktadha na kijiografia ya matumizi.

Msamiati wa lugha vipindi hubadilikabadilika kiasi kwamba ule wa awali husahaulika na mwingine wenye maana sawa kwa dhana au kitajwa kilekile huundwa na watumiaji “asilia” wa lugha hizo vipindi. Jambo hili hutokea zaidi katika lugha vipindi zilizoundwa kwa nia ya kuficha uhalifu au usimbeko mwingine wowote. Kwa msingi, watumizi wa lugha vipindi hujaribu kutumia msamiati usioweza kutambuliwa na watu wengi katika jamii lugha fulani ili kudumisha ule upekee wa kukundi cha wanalugha kipindi.

Ingawa lugha vipindi hujitokeza kama mali na hifadhi ya vikundi fulani fulani katika jamii lugha, wakati hufika ambapo lugha vipindi huenea na kuanza kutumika nje ya mipaka ya wazungumzaji asilia. Kwa mfano, lugha kipindi ya Sheng nchini Kenya hapo awali ilitumika kama lugha ya vijana kutoka tabaka la kati jijini Nairobi; sasa hivi lugha hii hutumiwa na watoto, vijana, watu wa makamo, na hata wazee wa matabaka yote, mijini na hata mashambani. Kwa hali hii, inadhihirika kuwa kadiri muda unavyozidi kupita lugha vipindi huweza kukiuka sifa yake ya kimsingi ya kuwa lugha inayotumiwa na kikundi fulani tu cha Watu katika jamii lugha kama vile vijana, wafungwa, wanamuziki, masenge, wasagaji, watumizi wa dawa za kulevya na wengineo.

Ifahamike pia kuwa lugha vipindi moja huweza kudhihirisha tofauti za hapa na pale kimuuundo hasa kutegemea masiala kama vile tofauti za kikabila, kitabaka na kimaeneo. Kwa mfano Sheng inayotumika mjini Nakuru ni tofauti na Sheng inayotumika mjini Nairobi na mjini Kisumu. Tukirejelea lugha ya Sheng mjini Nakuru maneno ya Kikikuyu yatatumika zaidi na katika mji wa Kisumu maneno ya Kidholuo yatatumika zaidi. Kwa mfano, jina *guthie* la Kikikuyu huzaa jina *mthii (*msafiri) kutokana kitenzi enda.

Watafiti waliowahi kuzitafiti lugha vipindi hueleza kuwa msemo hutambuliwa kuwa ni lugha kipindi kama una sifa mbili au zaidi ya hizi zifuatazo;

i. Upunguzaji wa hadhi au ubora wa lugha asilia ambayo ni mzazi kwayo au lugha rasmi fulani. Hali hii ya kupunguzwa ubora au hadhi huweza kujitokeza kimmandishi au kimazungumzo ambapo lugha inayotumika katika mawasiliano huonekana kama iliyo na matumizi mabaya ya lugha husika.
ii. Mtumiaji wa lugha husika akiwa anaifahamu na pia kufahamu kile kinachomaanishwa na watumiaji wengine wa lugha hii husika.
iii. Kuwapo kwa maneno fulani fulani ambayo yanatumiwa na kikundi cha watumiaji lugha husika kama visawe au sinonimu kwa maneno ya kawaida nia ikiwa ni kuficha ukweli uliozoeleka au kupunguza makali katika lugha husika na kwa hiyo kujitokeza na tasfida.

Kimsingi, lugha vipindi hutumiwa zaidi kama vyombo vya mawasiliano nia ikiwa ni kuunganisha kikundi fulani cha watu katika jamii lugha fulani kuliko kuwa kizuizi cha mawasiliano. Yaani, matumizi ya lugha vipindi huonyesha umoja, mshikamano na utambulisho wa kikundi husika na kwa matumizi ya lugha ya aina hii kuweza kutambuana kwa urahisi na pia kuwatenganisha na wale wasio kuwa katika kundi lao.

Sheng mjini Nakuru imeweza kujibainisha hasa lugha ya vijana na wanaitumia katika mawasiliano yao na katika kutekeleza shughuli zao mbalimbali za kila siku. Mjini Nakuru lugha hii ya Sheng sasa hivi hutumiwa kwenye magari ya usafiri wa umma,

kwenye muziki hasa ule pendwa na wa makabwela, kwenye mazungumzo ya kawaida ya kila siku na hata kwenye redio na televisheni.

Lugha kipindi Sheng imeweza kujitokeza kama chombo cha mawasiliano chenye umuhimu mkubwa sana kwa jamii ya Wakenya hasa vijana wa mjini Nakuru. Kupitia lugha hii ya vijana, Sheng inatumika katika kampeni za jinsi ya kuzuia mimba za mapema, umuhimu wa matumizi ya dawa za upangaji uzazi, kuzuia kuenea na hata kuangamiza ugonjwa hatari wa Ukimwi. Mifano ya maneno ya Sheng yanayotumiwa ni kama ifuatavyo:

i. *Chilli* kwa maana usifanye mapenzi nje ya ndoa.
ii. *Wacha mpango wa kando* kwa maana ya kuwa mwamififu katika ndoa yako.
iii. *Chukua control* kwa maana ya usiyahatarishe maisha yako kwa kufanya mambo yanayoweza kusabisha ugonjwa wa UKIMWI.

Lugha ya Sheng mjini Nakuru imejitokeza kama chombo imara cha mawasiliano ambacho kinatumika kwingi ili kufahamisha, kuelimisha na kuburudisha kiasi cha kwamba inatumika katika vyombo vya habari kama vile redio.

### 3.1.2. Hali na Hadhi ya Sheng Mjini Nakuru

Katika isimu jamii udaiglosia ni ile hali ya lahaja mbili tofauti kutumiwa katika jamii lugha iliyo na umojalugha au lugha mbili kutumika kimawasiliano huku kila moja ikipewa hadhi na majukumu tofauti tofauti.

**Hali na hadhi za lugha tofauti tofauti mjini Nakuru**

**Tanbihi**

**Wtf-watafitiwa**

1. **Hadhi ya juu zaidi**
2. **Hadhi ya juu**
3. **Hadhi ya chini**
4. **Hadhi ya chini zaidi**

**<u>Jedwali la kwanza</u>**

| **Wtf** | **Kiingereza** | **Kiswahili** | **Za kienyeji** | **Sheng** |
|---|---|---|---|---|
| i | 1 | 2 | 4 | 3 |
| ii | 1 | 2 | 3 | 4 |
| iii | 2 | 3 | 1 | 4 |
| iv | 1 | 2 | 4 | 4 |
| v | 1 | 2 | 3 | 3 |
| vi | 2 | 1 | 4 | 4 |
| vii | 2 | 1 | 3 | 3 |
| viii | 1 | 2 | 4 | 4 |
| ix | 2 | 1 | 3 | 3 |
| x | 1 | 2 | 4 | 4 |
| xi | 1 | 2 | 3 | 3 |
| xii | 2 | 1 | 3 | 3 |
| xiii | 1 | 2 | 3 | 3 |
| xiv | 1 | 2 | 4 | 4 |
| xv | 2 | 1 | 3 | 3 |
| xvi | 1 | 2 | 4 | 4 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| xvii | 1 | 2 | 3 | 3 |
| xviii | 2 | 1 | 4 | 4 |

Katika jedwali hili:

**Lugha ya Kiingereza.**

$^{10}/_{18}$ ya watafitiwa ilisema kuwa lugha ya Kiingereza ni ya hadhi ya kwanza na hii ni asilimia 55.6 ya jumla ya watafitiwa.

$^{8}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha ya Kiingereza ni ya hadhi ya pili na hii ni asilimia 44.4 ya jumla ya watafitiwa.

**Lugha ya Kiswahili.**

$^{6}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha ya Kiswahili ni ya hadhi ya kwanza na hii ni asilimia 33.3 ya jumla ya watafitiwa.

$^{11}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha ya Kiswahili ni ya hadhi ya pili nahii ni asilimia 66.1 ya watafitiwa.

$^{1}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha ya Kiswahili ni ya hadhi ya tatu na hii ni asilimia 5.6 ya watafitiwa.

**Lugha za Kienyeji.**

$^{1}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha za Kienyeji zina hadhi ya kwanza na hii ni asilimia 5.6 ya watafitiwa.

$^{8}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha za kienyeji zina hadhi ya tatu na hii ni asilimia 44.4 ya watafitiwa.

$^{9}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha za kienyeji zina hadhi ya nne na hii ni asilimia 50 ya watafitiwa.

**Sheng**

$^{9}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha ya Sheng ni ya hadhi ya tatu na hii ni asilimia 50 ya watafitiwa.

$^{9}/_{18}$ ya watafitiwa ilieleza kuwa lugha ya Sheng ni ya hadhi ya nne na hii ni asilimia 50 ya watafitiwa.

Hii ni kumaanisha kuwa lugha mjini Nakuru zinafuatana kama ifuatavyo kihadhi; kwanzia lugha ya hadhi ya juu zaidi hadi ya chini.

1. Kiingereza.
2. Kiswahili.
3. Sheng.
4. Lugha asili za Kiafrika.

Kulingana na jedwali hili Sheng imechukua nafasi ya lugha asili za kiafrika kulingana na mpangilio wa lugha kihadhi. Kulingana na jedwali la pili lugha za kienyeji zinachukuliwa kama zinazodidimia na nafasi yake kuchukuliwa na Sheng ambayo ni lugha inayokua.

### 3.2. Majukumu na matumizi ya “Sheng” mjini Nakuru

Luria (1960) ambaye ni mwana saikolojia anasema kuwa ili kufanikisha majukumu ya lugha ambayo yamekusudiwa kutumika na kutahini ukuaji, uendeleaji na uenezaji wa lugha hiyo kwa wahusika, huwa tunatofautisha majukumu manne makuu

Aliyaorodhesha hivi; lugha kama kifaa cha kujieleza, utendaji, mawasiliano na uwasilishaji wa mawazo na tajriba zetu. Kulingana na kauli hii ya Russian, Sheng ni chombo muhimu cha vijana katika kujieleza, kuwasiliana na kuwasilisha mawazo yao kwa wenzao.

Buliba na wenzake (2006:20) wanasema kwamba swala la lugha na utamaduni limetazamwa na wataalamu katika njia mbili. Kwanza, wanachukulia lugha kama chombo muhimu cha kueleza utamaduni wa jamii yoyote ile. Pili, kuna wale wanaoina lugha kama sehemu ya utamaduni wa jamii. Lugha ndiyo inayoonyesha jamii ninini, inaeleza watu wanaowasiliana wakitumia lugha hiyo. Imedokezwa kuwa mambo muhimu kuhusu maisha ya jamii ya watoto hupitishwa kwao kupitia kwa lugha, na kwa njia hii, mtoto hujifunza utamaduni wa jamii yake. Jambo hili linafanikishwa kupitia kwa maingiliano yake na wenzake, na kwa matumizi ya lugha ya kawaida akiwa nyumbani. Bulibana wenzake (2006) wanasema kuwa kuna mwigiliano mkubwa kati ya lugha, jamii na utamaduni. Kwa hiyo lugha ya Sheng ni muhimu sana mjini Nakuru kwa sababu inatuonyesha jamii ya vijana wanaohusiana na wanaoingilia kwa kuitumia kama jamii lugha yao na kama kitambulisho chao. Vijana huitumia sheng kama lugha yao ya

kawaida na hivyo kutuonyesha jamii ya vijana ni nini. Sheng ni chombo muhimu cha vijana kujiendeleza na kuuendeleza utamaduni wao.

Sheng ni muhimu sana katika maisha ya jamii ya vijana mjini Nakuru kwani kwa kuitumia vijana hueleza hisia zao, maoni na fikra zao. Sheng pia huchangia katika mwingiliano wa vijana na jamii.

**Tanbihi**

**Wtf - watafitiwa**

**A. Kiingereza**

**B. Kiswahili**

**C. lugha za kienyeji**

**D. lugha vipindi "Sheng"**

Je, ni lugha ipi huhusishwa na?

1- **wasomi**
2- **vijana**
3- **watu ambao hawajasoma**
4- **mawasiliano ya kawaida**
5- **Wazee**
6- **Mjini**
7- **Kupitwa na wakati**
8- **Usasa**

**9- Siasa**

**10- Biashara**

**11- Dawa za kulevya**

**12- Ukora**

**13- Ukabila**

**14- Ujuaji**

Wanafunzi 18 wa shule za upili mjini Nakuru walitafitiwa na maonbi yao yanajitokeza katika jedwali hili hapa chini.

**Jedwali la pili**

| wt | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| i | A,B | B | B | D | D | D | C | D | B | B | B | C | B | C |
| ii | A,B | D | C | B | C | D | C | D | A,B,C | B,A | D | D | C | D |
| iii | A | D | C | B | B,C | B | C | D | A,B,C,D | B | D | D | C | B |
| iv | A,B | D,B | B,C | C | C | B,D | C | D | B,C | B | D | D | C | D |
| v | A | D,A | C | B | C | D | C | D | A,B,C,D | B | D | D | C | D |
| vi | A | D | C | B,C | B,C | B,D | C | D | B | B | D | D | C | D |
| vii | A | D,A,B | B,C | B | C | A,B,D | C | D | B | B | D | D | C | D |
| viii | A,B | D | C | B | B,C | D | C | D | C,B | B,C | D | D | C | D |
| ix | A,B | D | C | C | B,C | D | C | D | B | B | D | D | C | D |
| x | A | D,B | C | C, | C | D | C | D | B | B,C | D | D | C | D |
| xi | A | D | C,B | C | C | D | C | D | B | B | D | D | C | D |
| xii | A | D,B | C,B | C | B | B,D | C | A,D | B | B | D | D | C | D |
| xii | A,B | D | C | B,C | C | B,D | C | D | C,B | D,B | D | D | C | D |
| xiv | A,B | D,B | C | C | B | D | C | D | B,C | B | D | D | C | D |
| xv | A | D | C,B | B,C | C | D | C | A,B | B,C | B,C | D | D | C | D |
| xvi | A,B | B | C,B | C | B | D | C | B | B | B,C | D | D | C | D |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| xvii | A | B | C | C | B | D | C | A | C | C | D | D | C | D |
| xviii | A | B | C | C | C | D | C | B | B,C | B | D | D | C | D |

Fomula ya kutafuta asimilia ya majibu kutokana na jedwali letu.

$^{n}/_{N}$ x 100

**Tanbihi**

n= jumla ya majibu ya watafitiwa.

N= jumla ya watafitiwa.

Kulingana na jedwali hili watafitiwa walieleza kuwa kila lugha huhusishwa na wahusika fulani. Ni bayana kuwa wahusika wanaoitumia lugha fulani huchangia sana katika lugha ile kupewa hadhi au kuitopeza.

Watafitiwa wetu ni 18 na ni wa kutoka shule sita za upili mjini Nakuru

Asilimia 68 ya wahojiwa ilieleza kuwa lugha zote ni muhimu na zinapaswa kutambulika Kenya kisheria na mjini Nakuru. Kutokana na jedwali hili, tunapata dhana ya udaglosia, utriglosia na ukwadriglosia mjini Nakuru. Kwa sababu ya hali ya wingilugha mjini Nakuru, lugha tofauti tofauti zinatumika katika mazingira tofauti na zimepewa hadhi tofauti kulingana na matumizi yake. Kila lugha ina kazi yake na mahali inapotumika.

Kulingana na jedwali letu la pili lugha tatu muhimu ambazo zilipewa nafasi za kwanza kwanza ni lugha ya Kiingereza, lugha ya Kiswahili na lugha ya Sheng na sababu ni kuwa lugha ya Kiingereza, ilichukuliwa kutumika sana katika nyanja mbalimbali mjini Nakuru haswa zile nyanja muhimu kama za kiteknolojia na kielimu. Asilimia 100 ya watafitiwa inahusisha lugha ya Kiingereza na wasomi, huku lugha ya Kiswahili nayo ikitumika sana

katika nyanja za kibiashara, ielimu na pia kwa kuunganisha makabila tofauti huku Sheng nayo ikionekana kama lugha muhimu ya kuwaunganisha vijana ambao ni sehemu muhimu katika jamii. Lugha za kiasili zilionekana kuwa muhimu kwa kuunganisha watu wa jamii moja na pia huleta hali ya kukubalika au kuitanishwa na jamii fulani, pia ni kitambulisho cha jamii lugha fulani. Asilimia 94 ya watafitiwa katika jedwali hili inaona lugha za kikabila kama zinazoleta ukabila na zinaonekana kama lugha ambazo zimepitwa na wakati.

Asilimi 100 ya watafiwa waliona lugha za kienyeji kama zinazodidimia haswa mijini nchini Kenya kwani wazazi wengi wanawafunza wana wao lugha ya Kiswahili na wanapotangamana na vijana wengine wanajifunza Sheng. Asilimia 94 waliziona kama lugha za watu ambao hawajasoma kwani kwa wakati mwingi hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine bila kupitia kisomo rasmi cha shuleni. Lugha ya Kiswahili na Sheng zinachukua nafasi ya lugha za kienyeji katika matumizi yake mijini nchini Kenya hasa katika mji wa Nakuru. Wazazi wengi wa wakati huu hawawafunzi wana wao lugha za kienyeji bali wengi wao huwafunza lugha ya Kiswahili na wengine huwafunza Kiingereza kama lugha yao ya kwanza hapa mjini.

Kama lugha za kienyeji huchukuliwa kama kitambulisho cha jamii lugha fulani, kwa nini Sheng isichukuliwe kama kitambulisho cha jamii ya vijana? Swali hii ni muhimu kwa sababu vijana ni sehemu muhimu katika jamii na utamaduni. Na ndio idadi kubwa ya watu wanaoishi mijini nchini Kenya, mmoja wapo ukiwa Nakuru.

### 3.3 **Majukumu ya Sheng**

### 3.3**.1Sheng kamaKitambulisho cha Vijana**

### 3.3.2 **Utambulisho**

Gumperz (1982) anaeleza juu ya mwingiliano wa kimawasiliano wa vikundi mbalimbali vya kisasa. Alieleza kuwa tukiwa binadamu tunachukua jinsia, kabila na tabaka kama vithibiti au mipaka ya kuunda vitambulisho vyetu vya kijamii. Kwa hiyo kulingana na utafiti wetu, Sheng ni lugha ya utambulisho wa vijana mjini Nakuru. Utambulisho huu husaidia kuingiliana sawa na maisha ya mjini yaani hutosheka na kujisikia sawa na maisha ya mjini Nakuru.

Lugha ya Sheng kama kitambulisho cha lugha miongoni mwa vijana mjini Nakuru haichagui wala kubagua vijana bora tu wa uweze kuitumia na kuielewa misamiati yake. Kila kijana hutaka na hupenda kujiskia akiwa mmoja wa kikundi fulani na ili atoshee katika kikundi lazima ajihusishe na mambo yanayounganisha kikundi hicho na lugha ni moja wapo ya mambo ambayo huwaunganisha binadamu. Kwa hivyo Sheng ni lugha ambayo huwaunganisha vijana wa matabaka na makabila mbalimbali mjini Nakuru.

Gile (1979) anaeleza kuwa utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi, lakini lugha hutumika katika mchakato huu kama ishara muhimu ya kueleza utambulisho huo husika. Kwa kauli hii, Sheng inaeleza utambulisho wa vijana kwa vijana na jamii nzima mjini Nakuru.

3.3.2**.1 Sheng hutumiwakuweka Siri**

Lugha tofauti tofauti huwa zimetengewa kazi tofauti tofauti na hutumika katika mazingira tofauti na miktadha tofauti katika jamii. Vijana hawatumii Sheng katika mawasiliano yao na wazazi wao au na walimu wao. Sababu ya wao kupenda Sheng ni kuwa wao huitumia ili kuficha mambo ambayo hawataki yaeleweke na wazazi na walimu.

Kuwepo kwa mtu ambaye vijana hawataki aelewe mawasiliano yao, huleta utumiaji wa lugha ya Sheng ili "kubana" mawasiliano yao ili asije akaelewa. Kubana huku kwa mawasiliano ni kwa kutumia lugha ambayo haieleweki na kila mtu. Kwa mfano lugha ya *Shelta* ambayo ilitumiwa na wasafiri ambao hawakutumia lugha ya Kiingereza sanifu wala Kiirishi sanifu. Walitumia *Shelta* kwa misingi ya kuweka mawasiliano yao fiche.

Kulingana na watafitiwa mambo ambayo vijana hawapendi yaeleweke na wazazi wao na walimu wao ni mambo yanayohusiana na uhusiano wao haswa wa kimapenzi, au uhusiano wa marafiki ambao huenda wazazi wao wasipendezwe na wao, matumizi ya mihadarati au mambo ya ukora, na katika Maisha ya shuleni huhusu jinsi vijana wanaendelea kimasomo au kama wamejihusisha na mambo ya upotovu wa nidhamu ambayo huenda yakapelekea wazazi wao au walimu waokukasirika na kuwachukulia hatua.Jedwali letu la pili linaeleza haya. Sheng ni lugha inayohusishwa na ukora, utumizi wa dawa za kulevya na haya ni mambo ya kisiri ambayo vijana hawangetaka wakubwa wao waelewe kama wanajihusisha nayo.

#### 3.3.2.2 Sheng huwaunganisha Vijana

Katika mji wa Nakuru vijana wametoka katika sehemu, matabaka na makabila tofauti tofauti nchini Kenya. Ingawa lugha ya Kiswahili ni ya taifa na huwaunganisha Wakenya wote, lugha ya Sheng huwaunganisha vijana wanaoishi mijini kote Kenya kama mjini Nakuru pasipo kubagua kabila, tabaka au jinsia. Shenghuwasaidia vijana kuuendeleza uhusiano wao hivyo basi husaidia katika ujenzi wa taifa na kuiendeleza amani. Sheng si lugha ya kikabila na husaidia katika kuzipenda na kuzihifadhi lugha nyingine kwa sababu hukopa maneno mengine kutoka kwa lugha ya Kiswahili na hata lugha za kienyeji.

Watafitiwa walieleza kuwa kwa sababu lugha ya Kiingereza na Kiswahili hutumika katika mazingira rasmi na kuonekana kama za kifahari wengi huchukulia Sheng mjini Nakuru kua duni. Hata hivyo ikiwa Sheng inaweza kupewa nafasina kutoonekana kama lugha ya vijana na inayohusishwa na majambazi, inaweza kuwa ya hadhi ya juu kiasi kiulinganishi kuliko ilivyo sasa. Hata hivyo kulingana na watafitiwa, hadhi yake sheng ni ya juu ikilinganishwa na lugha asili za Kiafrika. Haya yanajitokeza katika jedwali la pili ambapo lugha hii inahusishwa na vijana hiyo kuueleza umoja wao na kuunganishwa kwao na lugha hii.

#### 3.3.2.3 Sheng hurahisisha mawasiliano.

Miundo ya sentensi ya Sheng huwa ni sentensi sahili. Kwa kawaida sentensi hizi huwa fupi k.m. *amemuwahi vinoma* kwa maana *amempiga vibaya.*

Asilimia 78 ya vijana waliotafitiwa ilieleza kuwa haiwezi kujieleza kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa ufasaha na hivyo hubidi wachanganye lugha hizi au wajieleza kwa Sheng ili kurahisisha mawasiliano na kueleweka kwa urahisi. Ni lugha ambayo pia hurahisisha mawasiliano baina yao kwa sababu huitumia katika mazingira yote ikiwemo mazingira shuleni.

Sheng hutumika katika jumbe katika vibandiko magarini. Mifano ya vibandiko hivi ni:

i. *kadere ameiva* kwa maana *Dereva ni stadi au hodari*.

ii. *Karao alipe ndae* kwa maana *polisi alipe nauli*.

*iii.* *Wacha ugicagi! Ufala mob*! Kwa maana *wacha ushamba, ujinga mwingi.*

*iv.* *Kadere niaje tia meno mbili.* Kwa maana *dereva ongeza sauti ya redio*.

Matumizi ya Sheng katika vyombo vya habari huwavutia vijana. Wengi wao husikiliza stesheni zinazotumia Sheng na huvutiwa na vipindi vinavyotumia lugha hii. Wanasiasa wanatumia Sheng ili kuwavutia vijana katika kuwasikiliza ni njia ya kurahisisha mwingiliano na mwasiliano yao na vijana.

Ni lugha inayotumika katika muziki-pendwa na ingawa si wengi wanaoelewa jumbe zinazotokana na miziki hiyo, vijana huelewa na hurahisisha kupitisha ujumbe ambao ungekuwa na maneno machafu au yaliyo ya aibu. Kwa mujibi wa haya Sheng huficha ukali wa maneno ambayo huenda yasiwe ya heshima yakitumika hadharani. K.m.
*Cheki hizo wezere*kwa maana *anagalia hayo makalio*.

3.4**. Hitimisho.**

Lugha zote zina umuhimu kwani hujenga mawasiliano ya mtu binafsi na jamii nzima na hata huiendeleza jamii na nchi kwa ujumla.

Katika historia ya lugha Kenya ya sasa ni vyema kutambua Sheng kama kitambulisho cha vijana mijini nchini Kenya na kama iliyo muhimu zaidi kwani huwaunganisha.

Lugha ya Sheng inao mustakabali mwema kutokana na masiala mbalimbali. Kwanza ni kuwa ikiwa ni lugha ya vijana ambao idadi yao inazidi kukua kila uchao, lugha hii itakuwa na watumizi wengi. Pili ni kuwa kuna matumizi ya lugha hii kwenye vyombo vya habari kama vile redio na televisheni ambapo inatumiwa kwenye vipindi, matangazo ya kibiashara na kwenye muziki-pendwa.

Kwa wakati huu mjini Nakuru kuna watu wa makamo, hata wazazi, wanaowasiliana kwa kutumia Sheng. Majukumu ya Sheng yanaongezeka ikilinganishwa na hapo awali ambapo ilionekana tu kama lugha ya ukora.

# SURA YA NNE

# TOFAUTI YA MATUMIZI YA SHENG MJINI NAKURU

## 4.0. Utangulizi

Nadharia ya ufeministi inadai kuwa kijamii mwanamke na mwanamume wanayo majukumu tofauti tofauti katika lugha na umenke kwa mujibu wa Iribemwangi na Mukhwana (2011). Kuna namna jinsia huathiri lugha na lugha huathiri jinsia.

Inawezekana kuainisha msamiati wa lugha ambao ni maarufu kwa wanawake na msamiati ambao ni maarufu kwa wanaume ambao aghalabu hutofautiana kimaumbo, kimada, kimaudhui na kimatumizi. Hali hii ya lugha na jinsia inajitokeza vyema katika matumizi ya Sheng mjini Nakuru. Asilimia 91 ya watafiti wailisema kuwa jinsia inayopenda kutumia Sheng ni jinsia ya kiume kuliko ya kike. Sababu ya vijana wa kiume kutumia Sheng sana ni kuwa siri zao ni nyingi hasa siri zinazohusiana na matumizi ya mihadarati na mambo ya ukora. Kama ilivyo katika jedwali la pili Sheng ni lugha inayohusishwa na ukora na utumizi wa dawa za kulevya mambo ambayo hufanywa sana na jinsia ya kiume tofauti na matumizi ya Sheng kwa jinsia ya kike kama tutakavyoeleza hapo chini wakati tutashughulikia utofauti ulioko katika matumizi ya Sheng kwa jinsia tofauti.

Kuna utofauti ulioko katika matumizi ya Sheng mjini Nakuru na baadhi ya mambo ambayo huchangia katika jinsi Sheng inavyotumiwa ni;

1. Jinsi kila jinsia inavyotumia Sheng mjini Nakuru.
2. Matumizi ya lugha ya Sheng katika maeneo tofauti tofauti mjini Nakuru.

3. Mwelekeo wa vijana kuhusiana na lugha ya Sheng ambayo ni lugha ya mjini.

### 4.1. Tofauti ya Matumizi ya Sheng Kijinsia.

Lipo wazo miongoni mwa wanaisimujamii kuwa wanaume na wanawake wanazo lugha zenye kutofautiana kilimwengu katika vipengele mbalimbali vya muundo wa lugha mbali na hadhi.

#### 4.1.1. Matumizi ya Sheng kwa Jinsia ya Kike

Kulingana na utafiti huu wataafitiwa walieleza kuwa matumizi ya Sheng kwa jinsia ya kike huwa na sifa ya masengenyo, dharau, huruma, matumizi ya maneno yenye hisia, maneno yenye upole, kuzungumzia vitu vinavyowavutuia na wakati mwingine maneno yenye madharau. Mifano wa kwanza; masengenyo.

*Cheki yule mode anaboo, ametufika kooni, mamao zake hatushikanishi mpaka machepe hawagich any na maasaino ndio kibao*.

Kwa maana

*Mwangalie yule mwalimu hafurahishi na ametufika kwenye koo. Hisabati hatuelewi hata walio werevu hawaelewi chochote na kazi ya ziada ndiyo nyingi.*

Mfano wa pili; masengenyo/ dharau

*Yule demu hujidai na vile si supa kukiladi ako down na shepu ni mti mapera.*

Kwa maana

*Yule msichana ana maringo na hata si mrembo, kujivaa hajui na umbo lake la fanana na mti ya mapera yaani ni mwembamba sana.*

Mfano wa tatu; hisia za mapenzi

*Niliwai chali mchepe, anaspini na ameninoki vinoma.*

Kwa maana

*Nilimpata mvulana mwerevu, aliye na gari na ananipenda sana.*

Mfano wa nne; dharau

*Yule ndung'u alikuwa ananikatia nikamtia za zi.*

Kwa maana

*Yule mchuuzi alikuwa anataka niwe mpenzi wake nikamkataa.*

Mfano wa tano; hisia

*Eeeeh cheki ile ndula ni mwenda ile mbaya.*

Kwa maana

*Eeh angalia kile kiatu kinavutia sana.*

Mfano wa sita;huruma

*Woiye! cheki vile ako down masake alidedi.*

Kwa maana

*Angalia vile ana huzuni mamake aliaga.*

### 4.1.2. Matumizi ya Sheng kwa Jinsia ya Kiume

Lugha ya jinsia ya kiume huhusishwa na misamiati iliyo na sifa ya ubabe, ni lugha dhahania, iliyojaa matusi, majigambo, misamiati ya mihadarati na pombe.

Mifano ya matumizi ya Sheng kwa vijana wa kiume

Mfano wa kwanza; matusi

*Demu yule hujidai na ni poko.*

Kwa maana

*Msichana yule huringa na ni malaya.*

Mfano wa pili; majigambo

*Tulitei, tukachum stulla kisha tukajinaisi na tudem.*

Kwa maana

*Tulikunywa pombe, tukavuta bangi kisha tukafanya ngono na wasichana.*

Mfano wa tatu; majigambo

*Eeeh mademu wamenifia ile mbaya yaani siwakatii wao ndio wananidai*

Kwa maana

*Wasichana wanipenda sana yaani si mimi nawataka ndio wananiuliza*.

Mfano wa nne; ubabe

*Kasee kale kaliniletea umatha nikakanyaga vinoma.*

Kwa maana

*Mtu yule aliniletea ujinga nikamchapa vibaya.*

## 4.2. Tofauti ya Sheng Kimaeneo Mjini Nakuru

Katika mji wa Nakuru nilishughulikia matumizi ya "Sheng" katika mitaa mitatu ambayo haikabiriani: Mtaa wa Roda, Langa Langa na Shabaab

**Jedwali la tatu**

| **Maneno kwa Kiswahili sanifu** | **Shabaab** | **Rhoda** | **Langa langa** |
|---|---|---|---|
| Vaa nguo | Nikladi | Nijikwachue | Ning'are |
| Nyumbani | Crab | Base | Hau |
| Wazazi | Paro | Peroz | Paroz |
| Msichana | manzi | Demu | Chikile |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Matajiri | masonko | Masos | Mabola |
| Mihadarati | stulla | Widi | Shisha |
| Pombe | keg | Kanamba | Tei |
| Polisi | makarao | Mapae | Mablue |
| Matatu | mandae | manganya | mathree |
| Makalio | wezere | Rasa | Haga |

Kulingana na jedwali letu tunaona kuwa maneno yaliyo na maana moja yana majina tofauti katika maeneo haya tofauti. Kitabaka Langa Langa na Shabab zinakaribiana na Sheng yao huhusishwa sana na utingo na madereva. Roda ni mahali ambapo kitabaka ni pa hadhi ya chini.

Pia misamiati wa Sheng hutofautina katika maeneo haya. Roda ni mtaa ambao muktadha wa maneno yake utahusiana na maisha ya chini. Watu wa Shabab na Langalanga wana msamiati wao unaohusiana sana na maisha ya matatu, madereva na 'utingo.'

Hata hivyo kuna baadhi ya maneno ya Sheng ambayo yamekita mizizi katika matumizi yakena yanatumiwa na wengi mjini Nakuru. Wazee kwa vijana wanaielewa misamiati hii ya sheng.

Kwa mafano;

*Doo* kwa maana *pesa.*

*Manzi* kwa maana *msichana.*

*Chali* kwa maana *mvulana*

*Mbuyu* kwa maana *baba*

*Mathee* kwa maana *mama.*

*Mtoi* kwa maana *mtoto.*

### 4.3. Mwelekeo wa wanafunzi kuhusiana na Sheng

Vijana wengi nchini Kenya haswa kwenye miji ukiwemo mji wa Nakuru hupenda kuwasiliana wao kwa wao wakitumia Sheng na Engsh (Nzuga 2002, Mukhwana 1990, Abdulaziz na Osinde 1997).

Sheng hutumiwa na vijana wengine ambao hufanya kazi na katika matabaka yote ya kijamii. Hali ilivyo ya isimujamii nchini Kenya haswa katika miji ni kuwa ni vigumu kumpata binadamu aliye na umojalugha (Nzuga 2002). Hii inaweza kuwa sababu kulingana na Webb na Kembo-sure (2000:37) wanasema Sheng ni mchanganyiko wa lugha mijini nchini kenya.

Utafiti wetu ulitahini mwelekeo wa wanafunzi kuhusiana na Sheng na kama mwelekeo huu huchangia katika kubadilika kwa Sheng kimajukumu, kihadhi na pia hali ya lugha hii. Ni vyema kutambua kuwa mwelekeo wowote uwe chanya au hasi huchangia sana katika kuongeza au kushusha lugha kihadhi. Walimu na wazazi ni vyema watambue na waelewe mielekeo wa vijana kuhusu Sheng.

#### 4.3.1. Mwelekeo wa Sheng kimajukumu

Vijana wengi haswaasilimia 86 ya wanafunzi wa shule za upili ukilinganisha na vyuo vikuu hupenda kutumia Sheng hata katika mazingira ya shuleni kuliko lugha nyingine yoyote. Jedwali la nne linaloonyesha matokeo yetu, linaonyesha kuwa wengi wa vijana wanafurahia kutumia Sheng na wana mwelekeo chanya kwa matumizi yake katika mazingira ya shuleni, nyumbani na hata mjini.

Kulingana na jedwali la (3) asilimia 76 ya watafitiwa inaamini kuwa Sheng ni lugha ya usasa na asilimia 79 ya watafitiwa hufurahia kusikia wenzao wakiwasiliana kwa kutumia Sheng; asilimia 60 ya watafitiwa ilikubali kuwa wao hutumia Sheng katika mazingira yote bora tu kuwe kuna wenzaowanao ielewa. Wanaitumia katika mazingira ya shuleni, nyumbani na pia kwenye miji. Asilimia 61 ya watafitiwa inafurahia kutumia Sheng kuliko lugha nyingine yoyote. Asilimia 33 ya watafitiwa iliona ni vyema walimu watumie Sheng panapofaa ilikuwawezesha kuelewa masomo na pia wakitumie kufanya masomo yawe ya kuvutia.

Hata hivyo asilimia 67 ya watafutiwa ilipinga matumizi ya Sheng katika masomo huenda ikaathiri masomo yao. Kwa jumla, kulikuwa na mwelekeo chanya kuhusiana na matumizi ya Sheng kama tutakavyoona baadaye katika kazi hii kutokana na maswali yetu.

**Mielekeo ya vijana kuhusiana na Sheng**

**Tanbihi**

**A**=Sheng ni lugha ya usasa, **B**=nafurahia kuwasiliana kwa Sheng kuliko lugha nyingine yoyote, **C**=natumia Sheng kwa sababu hutumiwa kwenye vyombo vya habari, **D**=natumia Sheng shuleni,**E**=natumia Sheng nyumbani, **F**=natumia Sheng mjini,**G**=natumia Sheng shuleni, **H**=walimu wanastahili kuwatia wanafunzi motisha katika kutumia Sheng shuleni, **I**=najiskia sawa nikitumia Sheng kuliko lugha yoyote ile, **J**=Sheng inastahili kuatambulika kikatiba, **K**=nafurahia kusikiliza watu wengine wakiwasiliana kwa Sheng.

**Jedwali nne**

| Vithibiti | Wanaokubali kabisa | wanaokubali | Wasio na uamuzi | wasiokubali | Wanaokataa kabisa | Asilimia kwa jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A | 20 | 22 | 5 | 5 | 8 | 100 |
| B | 17 | 17 | 5 | 14 | 7 | 100 |
| C | 7 | 7 | 9 | 21 | 16 | 100 |
| D | 4 | 5 | 3 | 23 | 25 | 100 |
| E | 11 | 10 | 5 | 17 | 17 | 100 |
| F | 8 | 11 | 5 | 21 | 15 | 100 |
| G | 19 | 16 | 7 | 9 | 9 | 100 |
| H | 5 | 6 | 5 | 11 | 33 | 100 |
| I | 9 | 9 | 3 | 11 | 28 | 100 |
| J | 16 | 19 | 6 | 10 | 9 | 100 |
| K | 16 | 9 | 6 | 10 | 19 | 100 |

Katika majadiliano na wakaaji wa Nakuru waliotafitiwa, lugha ya Kiingereza inachuliwa kama lugha ya watu walio na elimu ya ngazi ya juu. Pia huchukuliwa kama lugha ya watu wa tabaka la juu na huhusishwa na ‘Wazungu”kama vile watafitiwa walivyoeleza. Kwa sababu ni lugha ya mkoloni na kitaifa, lugha ya Kiingereza inachukuliwa kuwa ya kifahari na iliyo na hadhi ya juu.

Hata hivyo, wengi wa wanafunzi tuliojadiliana nao wakiwa watafitiwa walisema kuwa lugha hii imeathiriwa sana na lugha vipindi Sheng. Pia asilimia zaidi ya 60 ya watafitiwa ilikubali kutoweza kuwasiliana kwayo kwa ufasaha. Wengi wa wakaaji wa Nakuru walifurahishwa kwa kufanywa kwa lugha ya Kiswahili lugha rasmi ya pili tofauti na hapo awali ambapo ilikuwa ni lugha ya kitaifa tu,na lugha ya Kiingereza kuwa lugha rasmi

pekee kwani si wengi walioweza kujieleza kwa lugha ya Kiingereza katika mazingira rasmi.

Watafitiwa walieleza kuwa lugha ya Sheng ina ladha na inavutia kuliko lugha nyingine yoyote.

Kijumla mambo yafuatayo yalieleza mielekeo ya vijana kuhusiana na Sheng mjini Nakuru:

i. Ni lugha ambayo haina sheria na kanuni za kisarufi.
ii. Hutumiwa na watu ambao hawawezi kujieleza kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili na Kiingreza
iii. Hakuna matumizi mabaya ya neno lolote lile, bora tu yule mnayewasiliana naye anaelewa.
iv. Lugha ya Sheng hutegemea muktadha. Muktadha ukibadilika maana ya neno huenda ikabadilika.
v. Ni lugha ya mtaa ya 'walioharibika.'
vi. Ni lugha ya hadhi ya chini ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza.
vii. Ni lugha yenye ladha katika matumizi yake na imejaa chuku.
viii. Hutumiwa na kila tabaka kwa sababu hutumika sana katika mazingira ya mtaa.
ix. Ni lugha ya utambulisho na humika kama kitambulisho cha vijana.
x. Vijana wanaitumia kwa sababu hurahisisha mawasiliano yao. Hutumiwa na watu ambao wanataka kuweka siri na wengine wasielewe kinachozungumziwa.

xi. Ni lugha ambayo hurahisisha maingiliano miongoni mwa vijana.

xii. Ingawa kuna asilimia ya wakaaji wa mji wa Nakuru wanaoona Sheng kama lugha inayodidimia, vijana wanaiona kama lugha itakayokua na kuwa na hadhi zaidi kuliko wakati huu. Kuna makamusi ambayo yametolewa ya Sheng (Ireri Mbaabu 2003 na Moga na wenzake 2004). Wanamuziki wanatumia Sheng katika miziki yao k.m. *Nonini* na *Prezzo.*

xiii. Kutokana na kuchukua data wengi wa watafitiwa hawakuioni Sheng kama ni lugha. Katika hojaji katika nafasi ya kujaza umilisi wa lugha hakuna mtafiti aliyetaja kama mmilisi wa Sheng. Ni wakati tu mtafiti aliuliza kuhusu Sheng ndio walijibu ni lugha ya vijana. David Mailu ni mmoja wa wakenya ambao wameandika noveli na kwa lugha ya Sheng.

xiv. Mwelekeo kuhusiana na Sheng unaweza kuwa katika kategoria tatu; mwelekeo chanya, mwelekeo wastani, mwelekeo hasi.

xv. Hii iliweza kuchanganuliwa kulingana na jinsi watafitiwa walifirikia Sheng ni au sio. Haya yalichangiwa na majukumu na mambo Sheng iliweza kutend au kutotenda kama lugha na kama chombo cha mawasiliano.

xvi. Matumizi ya sinonimu huleta usanii ambao huvunja uzoevu wa matumizi ya maneno kwa namna moja ingawa matumizi ya sinonimu hufanya lugha misamiati ya maneno mengine yasidumu.

xvii. Sheng huletea uhai maneno mengine ambayo huenda yakasahaulika k.m. matumizi ya neno *kupe.*

### 4.4 Hitimisho.

Matumizi ya lugha ya Sheng hutofautiana sana kimuktadha, kimatumizi, kimsamiati, kimuundo na kisarufi kulingana na jinsia, maeneo na mazingira ambayo lugha husika inatumika.

Namna watu wa eneo fulani wanavyotumia lugha ya Sheng mjini Nakuru ni tofauti na matumizi katika eneo lingine. Sura hii imeshughulikia namna jinsia ya kiume na ya kike inavyotumia lugha kwa njia tofauti katika sarufi, utamkaji wa maneno, uchaguzi wa msamiati, kiasi cha kuzungumza, mada zinazozungumziwa, mikakati ya jisia ya kuwasiliana, matumizi ya maneno ya miko na mbeko, upole na uhakiki katika matumizi ya lugha. Hata hivyo kuna baadhi ya maneno ambayo yanatumika katika mazingira yote watu wote na yanatumiwa na jinsia zote.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.1. Utangulizi

Sura hii ya mwisho kwa kifupi ni muhstasari wa matokeo, mapendekezo, mipaka ya utafiti na kutoa rai kwa utafiti zaidi wa baadaye. Utafiti wetu ulihusianana hali, hadhi na majukumu ya Shengmjini Nakuru. Nilikusanya data kutoka shule tano za upili mjini Nakuru. Watafitiwa walijaza hojaji kulingana na jinsi walivyoelekezwa.

### 5.2. Muktasari wa matokeo

Utafiti huu ulikuwa juu ya uchunguzi wa hali, hadhi na majukumu ya Sheng mjini Nakuru. Uliegemea kutambulisha hali, hadhi na majukumu ya lugha mbalimbali na ulijikita kikamilifu katika nadharia inayodai kuwa. Jinsi mhusika anavyopata lugha na vile anavyoingiliana na binadamu wengine humpelekea kujihusisha na kikundi fulani, cha wahusika fulani katika jamii. Wanajamii hutumia lugha fulani kama kitambulisho chao. Utafiti wetu uliongozwa na maswali haya na mengine;

i) Shengina majukumu yepi katika jamii?

ii) Hadhi ya lugha mbalimbali hutofautiana vipi?

iii) Kuna tofauti katika matumizi ya Sheng kimakazi, kimaeneo na kijinsia?

Kutokana na data tuliyokusanya na matokeo ya uchanganuzi, tulibaini bayana kuwa lugha tofauti, hutofautiana kimajukumu na kihadhi. Kunao ushahidi vile vile wenye mashiko kuwa jinsi watu wanavyoipata lugha na mwingiliano wa wahusika huchangia

sana kuipa majukumu na hadhi lugha husika. Utafiti wetu uliweza kubainisha kuwa katika matumizi ya lugha wahusika wanaoitumia lugha fulani ni muhimu sana. Kwa mfano: tuliona lugha inayotumiwa na wasomi na ya rasmi inaonekana kuwa ya hadhi ya juu ukilinganisha na lugha inayotumiwa nyumbani na katika maongezi ya kawaida.

Ufumbuzi mwingine tuliouibua ni kuwa wingi wa utumiaji lugha huwezesha kusambaa kwa ile lugha. Sababu ya lugha vipindi Shengkukua ni utumiaji wa lugha hii kwa wingi haswa miongoni mwa vijana ambao ndio wengi mijini nchini Kenya.Uelewawa lugha inayohusika na inayohusishwa na kikundi fulani ni muhimu sana kwa sababu uelewa huu husaidia katika kukua au kutokua kwa lugha husika.

Utafiti huu ulitokea kutambua kuwa matumizi ya hojaji huenda yakawa magumu kwani watafitiwa huenda wasiyajibu maswali yote hasa kama kuna yale yanayotokea kuzua mihemko zaidi. Watafitiwa wengine walitokea kuyajibu maswali kwa njia ya usemi wa taarifa kinyume na usemi halisi; kwa sababu hii ilitubidi kuwaongoza watafitiwa kabla ya kuanza kuyajibu maswali.

Utafiti huu ni hatua ya kuuelekea mtazamo chanya kuhusiana na matumizi ya lugha vipindi Sheng kwani utapelekea kukabiliana na maswala vyeti kikamilifu ikiwa jambo fulani litatakiwa kuwafikia watumizi wa lugha hii. Swala la muda lilikuwa pingamizi kwani kazi nyingi niliifanya mbali na chuo kikuu, hivyo basi ilinibidi kuhakikisha kuwa ninakabiliana na hali ngumu huko mashinani.

## 5.3. Pendekezo zaidi

Utafiti huu ulionyesha kuwa vijana wanao mwelekeo chanya kuhusiana na matumizi ya Sheng. Ni lugha ambayo inawaunganisha na iliyo na ladha katika matumizi. Hata hivyo, napendekeza wazazi na walimu wachangie katika utumiaji wa Sheng ili iache kuonekana kama lugha iliyojaa uchafu, inayohusishwa na ukora, ujambazi na dawa za kulevya.Hakuna lugha isiyo na matumizi ya kisiri kwa namna moja au nyingine na kila lugha huwa na maneno 'machafu' ambayo kwa wakati mwingi hayawezi kutumika hadharani.

Pendekezo lingine ni kama lile lilohusiana na Jwan na Ogechi (2004) linalohusiana na sera ya lugha haswa kwa jamii iliyo na wingilugha. Sera hii inapaswa ishughulikie watoto wanaozaliwa mijini haswa kwenye mitaa ambayo Sheng hutumiwa sana. Kwa sababu vijana wanaokua wakiwa kwenye miji na mitaa ni wa utumiaji wa Sheng hutokana na kuishi mijini. Lugha hii ya Sheng inapaswa ipewe nafasi kwa sababu kuipa nafasi na kuitambua ni kuwatambua wahusika wanaoishi mijini na haswa kwenye mitaa na kwenye vitongoji duni. Kwa hiyo utafiti wetu unatoa mapendekezo yafuatayo kuhusiana na mada yetu ya utafiti:

i. Utafiti ufanywe mjini Nakuru ili kubaini kama kuna hali ya hadhi na majukumu ya lugha iliyo ya pentaglosia.

ii. Utafiti ufanywe ili kubaini nafasi ya Sheng katika suala zima la upangaji lugha mjini Nakuru hasa kwa kurejelea mawazo ya Rubin na Jernudd (1971) kuhusu kama kweli lugha yaweza kupangwa au inajipanga yenyewe.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M. Osinde, K. (1997). Sheng and Engsh in Nairobi. *International journal of the sociology of language 125:1-2.*

Abdulaziz, M. (1978). *Evaluation report on survey of language use and language teaching in Eastern Africa* s.l: s.n.

Bosire, M. (2008). Sheng The Phonological, Morphological and Social profile of an urban vernacular. Tasnifu ya uzamili university of Albany; State University.

Bosire, M. (2009). What makes a Sheng word uniquelexical manipulation in mixed language? *Selected proceedings of th 39th annual conference on African linguistics somervile M.A.*

Buliba, A, Njogu, K na Mwihaki, A (2006). *Isimu jamii kwa wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi; Jomo Kenyatta Foundation.

Block, D. (2007). *Second language Identities, London*: Continuum.

Echessa, P,G (1990). A study of the word structure and processes involved in word formation in Sheng: *A case study of Eastlands area in Nairobi: Tasnifu* ya Uzamili ambayo haijachapishwa.

Fergusson, C.A. (1977). *Linguistic as Anthropology*. In Saville-Trioke (Ed) 1-1.

Fromkin, V.Rodman, R (1988). *Introduction to Language*. Holt: Rinechart and Winston

Fromkin, V. Rodman, R. and Hymes, N. (2003). *An Introduction to Language*. (7thed.) Boston: Wardsworth Thospson Corporation.

Giles, H. (1979). *Ethinicity Markers in speech.* Katika Scheres, K.R. na Giles, H. (whr.), *Social Markers in Speech*. London; Cambridge University Press.

Githiora, C (2002). Sheng: Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? *Journal of African studies: 15(2): 159-181.*

Gumperz, J.J. (Ed) 1982b). *Language and social Identity*. Cambridge; Cambridge University Press.

Hudson (1995). *Language and society*. London; Macmillan Publishers.

Iribemwangina Mukhwana. (2011). *Isimu Jamii*. Nairobi; Focus Publishers.

Karanja, L (2010). *Homeless at home. Linguistic, culture ana identity, Hubridity and Third space positioning of Kenyan urban youth*. Education canadienne et international, 39(2) 1-10.

Kembo-sure (1992)*The coming of ShengEnglish Today* 26-28.

Kiessling, R. na Mous, M. (2001). Urban Younth Language in African. *Paper presented at the conference on Language, Migration and the City,* November 22-24, 2001. Bayreuth: University of Bayreuth.

King'ei K. (2001). Language and Identity: The challenge of Sheng in Kenya. *Paper presented at the Association of Third World studies conference,* September 17-19, 2000. Njoro; Egerton University, Kenya.

Krashen, S. (1987). *Principles and Practice in Second Language Acquisition.* London: Prentice-Hall.

Labov, W. (1972a). *Sociolinguistic Patterns*. Philadelphia: Pennnsylvania University Press, Oxford: Black Well.

Lesley Milroy (1980) *Language and Social Networks*: University Park Press.

Mazrui, A.M. (1995). Slang and Code Switching; *The Case of Sheng in Kenya Africanistische Arbeispapier 42:168-179.*

Mazrui, A.M. na Mphande, L (1990). How is a code mixes grammar organized? Evidence from Sheng.*Paper presented at the 21st Annual conference on African linguistics,* April 12-14, 1990.

Mbaabu et al (2003). *Sheng-English Dictionary*, Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University.

Moja, J. and Danfee (2004). (eds) *Sheng Dictionary.* Ginseng Publishers, Nairobi. 2004.

Mukhwana, A. (2008). Language Attitudes in Nairobi, Mombasa and Kisumu. Tasnifu ya uzamifu ambayo bado haijachapishwa.

Myers-scotton, E (1993). *Social Motivation for Code Switching*; Evidence from Africa.Oxford Ctarendon Press.

Ngesa, M. (2002). AndSheng Lives on…*profile*. East African Standard.

Nzuga na Kibande, M.P *Sheng and Engsh : The Booming offspring of linguistic intermarriage* in contact Ingrid Rissone (ed) Bayreuth Africa studies 51. 2002.

Ogechi, N.O. (2002). Trilingual Code-Switching in Kenya. Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng.tasnifu ya Uzamifu ambayo bado haijachapishwa. Hamburg: University of Hamburg.

Ongechi, N.O. (2005.) On Lexicolization in Sheng. *Nordic Journal of African Studies*. 14(3), 334-355.

Osinde, K. (1986). Sheng; An Investigation into the Social and structural Aspects of an Avolving language.Tasnifu ya B.A ambayo bado haijachapishwa.Nairobi; University of Nairobi.

Peter, S. Well (2002). *Socialinguistics*. Routledge; London.

Rubin Joan and Jernudd, B.H (ed). *Can language be planned?* The university press of Hawaii 1971.

Samper, H. (2002). Taking Sheng: The role of a hybrid language in the construction of identity in youth culture in Nairobi, Kenya. Tasnifu ya Uzamifu ambayo bado haijachapishwa.University of Pennsylvania.

Shitemi, N.L. (2002). Pidginization: Sheng the Melting-Pot of the Kenyan Language and anti-Babel development. *Kiswahili* 64:1-15.

Spyropouloss, M. (1987). Sheng: Some Preliminary Investigation into a recently Emerged Nairobi Street Language: *journal of the Anthropological society of Oxford*. 18(2): 125-136.

Trudgill, P. (2000). *Socialinguistic Variation and Change*. Edinburgh: Edniburg University Press.

Tuki (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Waithira, C. (2001). .*A Study of the Structure of the Youth Jargons in Nairobi*: M. Phil. Thesis. Eldoret; Moi University.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Warambo P. (2011). Uchanganuzi wa Maendeleo ya Kisemantiki katika Sheng; Mtazamo wa kipragmantiki.

Webb, M.N (1993). *Miaka 50 katika jela*. Nairobi; Heinman Kenya.

Pragmatiki Leksika. Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa.University of Nairobi.

## KIAMBATISHO A: HOJAJI

**UTAFITI WA HALI, HADHI NA MAJUKUMU YA SHENG MJINI NAKURU.**

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya umahiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi ambapo nasomea lugha ya Kiswahili. Zipo tetesi kuwa Sheng inaharisi sana ukuaji mwema wa lugha ya Kiswahili. Nimekuja kwako ili nikuombe unijazie hojaji hii ili nijue hali halisi ya lugha ya " Sheng" hasa mjini Nakuru. Majibu yako yatasaidia kuiboresha kazi yangu na kuipa mwelekeo na mkabala. Majibu yako yatakuwa ni ya siri sana na wala hayatatolewa kwa yeyote.

**SEHEMU A: MAELEZO KUHUSU MTAFITIWA**

1. Jinsia ___________________________________
2. Kiwango cha elimu_________________________
3. Umri____________________________________
4. Shule/Chuo_______________________________
5. Umilisi walugha. Wewe ni msemaji ni lugha zipi? (Zitaje zote kwa namna unavyozichangamkia.)

**SEHEMU B:**

Matumizi ya lugha katika jamii ni jambo ambalo halina budi kutimizwa. Lugha mbalimbali hutumika katika nyanja tofauti tofauti. Kama mhusika katika jamii utakabiliana vipi na maswala haya? (**ELEZA KWA USEMI HALISI.)**

1. Kwa maoni yako, Shengni nini?

2. Sheng hutumiwa na akina nani?
3. Kwa nini Sheng hutumiwa?
4. Sheng hutumiwa sana na jinsia gani? (Ya kike au kiume?)
5. Kwa sababu gani?
6. Je, matumizi ya Sheng hutofautiana kulingana na jinsia?
7. Shengina hadhi gani katika jamii ya mjini Nakuru? (Ya juu au ya chini?)
8. Kwa nini hadhi ya sheng iwe jinsi ilivyoeleza hapa juu?
9. Taja majikumu ya Sheng kama inavyotumika mjini Nakuru
10. Je Sheng hutofautiana kimatumizi katika maeneo mbalimbali mjini Nakuru?
11. Kama hutofautiana, toa mifano jinsi ambavyo Sheng hutofautiana.
12. Kulingana na maoni yako, panga lugha zifuatazo kihadhi, kwanzia ya juu hadi ya chini

a) Lugha za kikabila
b) Lugha ya Kiingereza
c) Lugha ya Kiswahili
d) Sheng
e) Lugha nyingine yoyote unayoifahamu

13. Sheng hutumika wapi? (Ofisini, nyumbani, mitaani au shuleni?)
14. Hutumiwa na kina nani na kwa nini?
15. Je sheng ni Lugha ambayo inakua au inadidimia?
16. Lugha gani huhusishwa na:

a) Wasomi
b) Vijana

c) Watu ambao hawajasoma

d) Mawasiliano ya kawaida

e) Wazee

f) Watu wa mjini

g) Kupitwa na wakati

h) Usasa

i) Siasa

j) Biashara

k) Dawa za kulevya

l) Ukora

m) Ukabila

n) Ujuaji